# Nipashe

Jumatatu Agosti 22, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581045

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW




**WANASOKA 7 WENYE NDEGE KALI BINAFSI**

UKURASA 12








**Mtoto** wa waziri aendelea kusota mahabusu, polisi wataja kinachojiri

UKURASA 4

TANZANIA SENSA 23 Agosti 2022 Jiandae Kuhesabiwa



1944 - 2022

# SIMANZI

- **Samia**, vyama vya siasa wamlilia Mrema, mke wake ateta na Nipashe...

*Endelea ukurasa 2*



## YALIYOMO


UKURASA WA 5

**TRA YAWEKWA MTEGONI LESENI KWA MADEREVA**

KAMANDA wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Wilbrod Mutafungwa...


## Anusurika kifo wakati akijifungua kwa mganga wa jadi

UKURASA 3




Ofisa Mkuu wa Rasilimaliwatu Benki ya NMB, Emmanuel Akonaay (kushoto), akimkabidhi mfano wa hundi ya Sh. milioni 20 Waziri wa Maliasili na Utalii, Balozi Dk. Pindi Chana (wa pili kushoto), kwa ajili ya ufadhili wa mafunzo kwa wadau wa mnyororo wa thamani kwenye sekta ya utalii. Kulia ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Chuo cha Utalii Tanzania (NCT), Dk. Shogo Mlozi na Kamishna Jenerali wa Uhamiaji, Dk. Anna Makakala. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Serikali yatoa ufafanuzi ajira makarani wa sensa

UKURASA 4


**MICHEZO** **DEJAN: SIMBA MTAFURAHI SANA** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

# Simanzi kifo cha Augustino Mrema

**Na Waandishi Wetu**

SIMANZI imetawala kwa wadau wa siasa nchini kutokana na kifo cha Mwenyekiti wa Tanzania Labour Party (TLP), Augustino Mrema (77) kilichotokea jana asubuhi katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH).

Mrema ambaye katika siku za hivi karibuni alionekana kwenye majukwaa ya kijamii na siasa, alijadiliwa kwenye mitandao ya kijamii Machi mwaka huu alipotangaza kuoa na kufunga ndoa na Doreen Kimbi katika Kanisa Katoliki Parokia ya Uwomboni Kiraracha mkoani Kilimanjaro, Machi 24, mwaka huu.

Taarifa za kifo hicho zilithibitishwa na Msemaji wa MNH, Aminiel Eligaisha, aliyesema kuwa Mrema alilazwa hospitalini huko Agosti 16, mwaka huu na alifikwa na umauti jana saa 12:15 asubuhi.

Mke wa Mrema, Doreen alisema kifo cha mume wake kimemwacha katika wakati mgumu kwa kuwa ndoa yao ilikuwa imeanza kustawi, ikiwa na miezi minne na siku 28 na walikuwa naye hospitalini hadi dakika ya mwisho.

**SAMIA, WANASIASA**

Katika ukurasa wake wa Twitter, Rais Samia Suluhu Hassan aliandika jana: "Nimesikitishwa na kifo cha Mwenyekiti wa Chama cha TLP, Augustino Mrema kilichotokea leo asubuhi jijini Dar es Salaam. Nitamkumbuka kwa mchango wake katika mageuzi ya siasa, uzalendo na upendo kwa Watanzania. Pole kwa familia na wana TLP. Mungu amweke mahali pema. Amina."

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, pia alieleza kupokea kwa masikitiko taarifa za kifo cha Mrema, akisema: "Ikumbukwe Mrema alitoa mchango mkubwa kwa taifa katika mapambano dhidi ya wala rushwa. Mwenyezi Mungu ailaze roho ya marehemu mahala pema peponi, Amin."

Msajili wa Vyama vya Siasa, Jaji Fransis Mutungi, alisema: "Huwezi kuzungumzia siasa za Tanzania bila kumtaja Mrema, alitetea siasa, 'ali-balance' (uwiano) kwamba huwezi kubisha kila kitu, kuna ambavyo utakubaliana navyo, alisimama kutetea kile alichokiamini na kinachostahili bila kujali ataonekana vipi.

"Mrema alionyesha ukomavu mkubwa kwamba siasa ni kwa mustakabali wa nchi yetu, alijizolea mvuto wa aina yake, wengi walimtaja na kumpenda, wengi wanamkumbuka kwa Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1995 lakini siku zote alivutia kwa siasa zake na ameacha alama na chachu kubwa kwa siasa zetu."



Augustino Mrema alifunga ndoa na Dorin Kimbi Machi 24, mwaka huu.

**DAKIKA ZA MWISHO**

Mwenyekiti wa Kanda C, Emmanuel Matee, alisema Mrema alikuwa mwanajumuiya ya Bikra Maria Mama Rozari, aliyehamia Salasala Julai 17 mwaka 2021, akaomba kushiriki masuala ya kiimani na alivyojulishwa taratibu, alifanya misa ya shukrani Agosti 28 mwaka jana.

Alisema misa hiyo ilifanyika Parokia ya Salasala ikiwa ni shukrani kwa miaka 45 ya ndoa, miaka 76 ya kuzaliwa na watoto sita na wajukuu wanane aliojaliwa, ikifuatwa na ibada maalum nyumbani kwake iliyoongozwa na Padri Philibert Marando.

Alisema Mrema aliomba na kungama, kufanya malipizi, kominika na waliunganishwa akapata sakramenti na familia yake.

"Baada ya wiki moja (Septemba 17, 2021) mkewe Rose Mrema alifariki.

Hivi karibuni kabla ya kwenda hospitalini, aliniita tena (Mwenyekiti) akaniambia anataka kusafisha roho yake, akaomba Paroko wa Parokia ya Augustino Salasala, Padri Peter Assenga, aitwe na alikwenda nyumbani kwake kuanzia saa 10 jioni hadi usiku sana.

"Juzi niliongea naye akasema anajisikia vibaya, alipelekwa Muhimbili wiki iliyopita, niliienda kumtembelea Ijumaa iliyopita (Agosti 19), tukaongea sana akasema hali yake siyo mbaya sana, ila akaomba huduma ya kiimani, nikaonana na Sista Leopadia kwa ajili ya kitubio, ekaristi na upako mtakatifu.

"Mchana Padri akaenda akapata huduma zote, leo asubuhi nimesikia taarifa ya msiba, lakini tunamshukuru Mungu kwa maisha yake na hasa upatanisho na Mungu wake alioufanya, alipata nafasi ya kujiweka kwa Mungu kabla ya umauti."

Mbunge wa zamani wa Viti Maalum wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Kilimanjaro, Grace Kiwelu, amesema licha ya tofauti za kiitikadi, anamkumbuka zaidi Mrema kwa namna alivyokuwa hodari wa kufanya siasa zisizoumiza mwingine na ameacha alama kwenye uwanja wa siasa za kistaarabu.

Naibu Katibu Mkuu wa Chama cha NCCR Mageuzi, na aliyekuwa Mbunge wa Moshi Vijijini (CHADEMA) kwa kipindi cha miaka mitano kati ya 2015 na 2020, Athony Komu, alimwelezea Mrema kuwa alikuwa na mchango mkubwa kwenye siasa za vyama vingi nchini.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Kiraracha, Kata ya Marangu Magharibi, Thomas Mrema, alisema wamepata majonzi makubwa kwa kuwa kiongozi huyo alikuwa msaada kwao kwa miaka mingi na alikitangaza kijiji ndani na nje ya nchi.

"Tulikuwa hatuna shule ya msingi, kupitia michango yake tulijenga Shule ya Msingi Malang'a, watoto wetu wanasoma karibu, hawatembei umbali mrefu, pia alishiriki kuchangia afya na miundombinu hadi kwenye kanisa, alishirikiana nasi.

Pia alikuwa mwanasiasa hodari na mchapakazi ambaye aliongoza siasa za upinzani," alisema.

Katibu Mkuu wa TLP, Richard Lyimo, alisema chama kimepata pigo kubwa kuondokewa na Mrema ambaye alikuwa mwalimu wa walimu wa siasa za Tanzania na kwamba bendera za chama hicho zitapepea nusu mlingoti kwa siku 10.

Mwenyekiti wa Chama cha NCCR-Mageuzi, James Mbatia, anayeongoza chama ambacho Mrema aliwahi kugombea nafasi ya urais katika Uchaguzi Mkuu wa mwaka 1955, anasema kiongozi huyo ni nyota ya kwanza kung`arisha uchaguzi mkuu wa kwanza wa mfumo wa vyama vingi Tanzania mwaka 1995.

"Sisi NCCR-Mageuzi kwa pamoja tunampa sifa ya 'baba' kwani alikuwa mgombea wetu wa urais katika uchaguzi mkuu wa kwanza wa mfumo wa vyama vyingi vya siasa, mwaka 1995.

"Alikuwa wa kwanza kuonyesha kiu ya mageuzi iliyopo ndani ya Watanzania kwani uchaguzi ule ulisisimua wengi.

Katika uwanja wa siasa, hasa kwenye majukwaa ya kisiasa na bungeni, alionyesha uwezo wa kipekee wa kujenga hoja zenye kuibua tabasamu katika mioyo ya wasikilizaji," alisema Mbatia.

Mmoja wa waanzilishi wa NCCR-Mageuzi, Faustine Sungura, alisema kifo cha Mrema ni pigo kubwa kwa kuwa ndiye mwanasiasa aliyeupa nguvu upinzani nchini.

Sungura ambaye aliwahi kushika nyadhifa mbalimbali ndani ya NCCR Mageuzi, alisema TLP bila Mrema itakuwa na wakati mgumu kwani alikifunika kiasi kwamba viongozi wengine waliopo ndani ya chama hicho walikuwa hawaonekani.

Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa CHADEMA, John Mrema, katika salama za chama hicho kuhusu kifo cha Mrema jana, alisema:

"Alipokuwa serikalini, alikuwa kiongozi mwenye ushawishi mkubwa kwa makundi ya kijamii na ilifikia wakati akawa na uwezo wa kuagiza majambazi wasalimishe silaha na ikawa hivyo.

"Atakumbukwa pia kwa kuwa kiongozi wa ngazi za juu wakati huo, kujitoa kwenye chama tawala na kujiunga na upinzani na akayaishi maisha ya upinzani. Atakumbukwa kwa kupigania demokrasia ya mfumo wa vyama vingi na akayaishi maisha hayo mpaka umauti unamkuta.

"Mwaka 1995 alifanya kampeni ambazo ziliitikisa serikali na chama tawala na kufanikisha kupata kura nyingi za urais na kupata wabunge wengi katika uchaguzi wa kwanza wa mfumo wa vyama vingi nchini."

Naibu Katibu wa Habari, Uenezi na Uhusiano na Umma wa ACT-Wazalendo, Janeth Rithe, alisema chama hicho kinaungana na Watanzania wote kutoa pole kwa familia ya Mrema, chama chake cha TLP na Watanzania wote kwa msiba huo.

Mwenyekiti wa Chama cha Wananchi (CUF), Prof. Ibrahim Lipumba, alisema Mrema ni kiongozi atakayebaki kwenye rekodi za nchi kama kinara wa mapambano dhidi ya rushwa na ufisadi na kielelezo cha uwajibikaji akiwa ndani na CCM na baadaye akiwa upinzani kupitia Chama cha NCCR-Mageuzi kabla ya kuhamia TLP.

"Utendaji wake uliotukuka akiwa serikalini, ulimsukuma Rais wa awamu ya pili, Ali Hassan Mwinyi, kumuunganishia vyeo nje ya utaratibu wa kawaida uliozoeleka kabla na baada ya hapo.

"Ujasiri wake uliweka msingi mkubwa kwa wanasiasa wa upinzani nchini hususani kwa vijana katika miaka 10 ya mwanzo ya uchaguzi ndani ya mfumo wa vyama vingi nchini. Huu ni msiba mkubwa wa taifa letu.

"Kwa hakika Mrema kalitumikia taifa letu kwa uzalendo ndani ya mfumo wa chama kimoja na vyama vingi, alikuwa mvuto wa kisiasa wa kipekee kwa wananchi wa kawaida hasa mwaka 1995. Watanzania hatutasahau mchango wake katika siasa za vyama vingi," alisema.

**WASIFU WAKE**

Mrema alizaliwa Desemba 31, 1944 huko Vunjo mkoani Kilimanjaro. Aliwahi kuwa wa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na alihama kutoka CCM Februari 1995 na kujiunga na NCCR-Mageuzi na baadaye alijiunga na TLP.

Aliwahi kuwa Mbunge wa Vunjo mara kadhaa kabla ya kushindwa katika uchaguzi wa kitaifa na James Mbatia wa NCCR-Mageuzi mwaka 2015 na mwaka 2016 alichaguliwa na Rais wa awamu ya tano, Dk. John Magufuli kuwa Mwenyekiti wa Bodi ya Parole Tanzania.

Mrema alishika nyadhifa kadhaa serikalini, Shirika la Usalama wa Taifa na CCM tangu mwaka 1966. Nafasi zingine alizoshika ni pamoja na mwalimu wa uraia vijijini 1974-1980, Mwalimu Chuo cha Usalama wa Taifa 1980-1982, Naibu Ofisa Msaidizi wa Usalama wa Taifa Mkoa wa Dodoma 1982-1984, Naibu Mkuu wa Usalama Mkao wa Shinyanga (1985-1987).

Mrema ni mtoto wa pili kuzaliwa kati ya ndugu watano na ni wa kabila la wachaga wa Kijiji cha Kiraracha, karibu na Mlima Kilimanjaro.

Alisoma Shule ya Msingi na Sekondari mjini Moshi mwaka 1955 hadi 1963 kisha akajiunga na Chuo cha Ualimu cha Mtakatifu Patrick ambako alimaliza elimu yake ya sekondari mwaka 1965.

Aliendelea kielimu katika Chuo Kikuu cha Cambridge O-level mwaka 1968 kisha akajiunga na Chuo cha Elimu ya Siasa, Kivukoni.

**■Imeandaliwa na Elizabethi Zaya (DAR), Godfrey Mushi (ARUSHA) na Thobias Mwanakatwe (SINGIDA)**

KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

KING LION INVESTMENT LTD
ANATANGAZA
KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA KING LION YENYE NAMBA ZA USAJILI
MC 249 DAX
KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI
TAARIFA YA POLISI
KAH/RB/544/2022

# Anusurika kifo wakati alipokwenda kujifungua kwa mganga wa jadi

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

BINTI wa miaka 17 (jina linahifadhiwa), amenusurika kifo alipokwenda kwa mganga wa jadi kujifungua baada ya siku zake kupitiliza na mganga huyo kutumia dawa za mitishamba kumnywesha ili kuongeza uchungu na zingine kumwingiza kwenye njia ya uzazi na mtoto kushindwa kutoka.

Binti huyo mkazi wa Halmashauri ya Manispaa ya Kahama, alilazimika kukimbizwa kituo cha afya baada ya mganga huyo kushindwa kumzalisha na kutokomea kusikojulikana.

Pia imeelezwa kuwa mganga huyo alikuwa anaingiza dawa hizo kwenye njia ya uzazi zimsaidie kama ganzi.

Mratibu wa Afya ya Mama na Mtoto wa halmashauri hiyo, Caroline Maliseli, alibainisha hayo jana, wakati akizungumza na gazeti hili kuwa tukio hilo lilitokea Agosti 18, mwaka huu, baada ya mama mzazi wa binti huyo kukiri kwamba alikosa fedha ya nauli ya kumpeleka binti yake zahanati kujifungua.

Alisema mwanawe alipitiliza muda wake wa kujifungua wa miezi tisa na kuamua kumpeleka kwa mganga wa jadi kujifungua kienyeji.

Alisema walipofika kwa mganga huyo walipewa dawa za miti shamba za kuongeza uchungu na nyingine kuingiziwa sehemu za siri hali iliyomsababisha maumivu makali.

Kadhalika, wakati wanaendelea kumweka dawa hizo, mtoto alikuwa ameshachungulia katika njia yake ya uzazi akiwa ametanguliza uso na mganga huyo anadaiwa kuendelea kumsokomeza dawa hizo kwa vidole vyake vilivyokuwa vikimchoma mtoto mdomoni, usoni na puani.

Caroline alisema, baada ya hali hiyo binti huyo alizidiwa kutokana na maumivu makali na uchungu kuongezeka uliosababishwa dawa za miti shamba alizokuwa akisokomezwa.

Alisema, binti alikimbizwa Zahanati ya Mpera na hali ilivyozidi kuwa mbaya walimpeleka Kituo cha Afya cha Mwendakulima kwa matibabu zaidi.

Alipofikishwa kituoni hapo walibaini njia yake ya kawaida ilikuwa ndogo na mtoto kushindwa kupita hali iliyolazimu kumfanyia upasuaji na kumnusuru yeye na mtoto wake.

Mtoto alipotolewa alikutwa amevimba mdomo na pua kutokana na kuchomwa na vidole vya mganga wakati akimsokomeza dawa mama yake.

"Hali ya binti inaendelea kuimarika, lakini mtoto wake hawezi kunyonya kwa sababu aliumia midomo yake, tunaendelea na matibabu na hali yake itakapoimarika tutamkabidhi mama yake ili amnyonyeshe...Niombe waganga wa kienyeji kuacha kuingilia fani ambazo haziwahusu," alisisitiza Maliseli.

Mama mzazi wa binti huyo (jina linahifadhiwa), alisema mtoto wake alikuwa ameolewa Kijiji cha Mwajilingo, Nzega, mkoani Tabora na alipopata ujauzito na kukosa matunzo alikimbilia nyumbani kwake wakati huo alikuwa ameshapitiliza muda wa kujifungua.

Alisema, sababu ya kumpeleka kwa mganga huyo ni kukosa Sh. 15,000 na vitenge viwili.

Alidai kuwa hakujua madhara ya kumpeleka mwanawe kwenda kujifungua kwa mganga wa jadi na kuiomba serikali isimchukulie hatua.

Akiongea na Nipashe, binti huyo alisema anamshukuru Mungu amejifungua salama licha ya kufanyiwa upasuaji.

Ofisa Muuguzi wa Kituo cha Afya Mwendakulima, Christian Jackson alisema, alimpokea Maua akiwa katika hali mbaya na kama wangechelewa kumpatia huduma ya upasuaji angeweza kupoteza maisha yeye pamoja na mtoto wake tumboni.

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**PAULO LUCAS KWIDIKA** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 113 BPM.** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI

TAARIFA YA POLISI
**GEI/MBO /RB/ 327216 /2022**

## KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI

**SANLG WORLD WIDE** INVESTMENT ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI AINA YA SANLG YENYE NAMBA ZA USAJILI **MC 814 CKS** KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHOCHOTE CHA POLISI

TAARIFA YA POLISI
**KAH/RB/539/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ALLY IKOME MURUKE** anatanagza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba S0189-0015 kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **FEZA BOYS' SECONDARY SCHOOL** mwaka **2010.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/CEN/RB/90618/2022**

## KUPOTEA KWA CHETI



**ALLY IKOME MURUKE** anatanagza kupotea kwa cheti cha kidato cha sita chenye index namba **S0189-0509** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **FEZA BOYS' SECONDARY SCHOOL** mwaka **2013.** Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

**POLISI TAARIFA: DAR/CEN/RB/90618/2022**

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

BBN Limited TZA

## OMBI LA KUONESHA NIA KWA UTOAJI WA Mtambo wa Kutengeneza Zege na Malori ya Kusafirishia Zege

### KUMB : ETJ-BB-PE-EI-GEN-SI-0001-00.

BESIX Ballast Nedam Limited, MKANDARASI wa Uhandisi, Ununuzi na Ujenzi wa Gati na Vifaa vya Kupakia kwenye Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni na wataalamu wenye uzoefu kueleza nia zao kwa:

**Mtambo wa Kutengeneza Zege na Malori ya kusafirishia zege**
Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Kama sehemu ya mradi wa EACOP, mafuta ghafi yatapakiwa kwenye meli kupitia kituo kilicho karibu na ufukwe wa Bahari ya Hindi. Kituo hiki kitakuwa umbali wa kilomita 2 kutoka ufukweni, eneo la Hifadhi ya Baharini lililopo kwenye peninsula ya Chongoleani mbele ya Bandari ya Tanga nchini Tanzania.

**WIGO WA VIFAA / HUDUMA:**

1. **Mtambo wa kutengeneza Zege:**
Kutafuta makampuni yenye mtambo wa kuzalisha takribani m3 3500 za zege kati ya Januari 2023 na Juni 2024.
2. **Malori ya kusafirishia zege:**
Kutafuta makampuni ambayo yanaweza kukodisha lori za kusafirishiaa / kubeba zege.

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**
Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa kuonyesha:

- Orodha ya uzoefu, rekodi za miradi inayoonyesha uzoefu katika kutengeneza na kusambaza zege.
- Wafanyakazi waliohitimu na kuthibitishwa kufanya kazi za kuthibiti Ubora/ Kuthibitisha Ubora (QA/QC)
- Mtambo wa kuzalisha Zege uliokaguliwa na kuthibitishwa Ubora (Hati ya Ubora ya Ulaya au Tanzania);
- Wasifu wa kampuni wenye uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha na rasilimali za kutosha kusimamia kandarasi husika.
- Sera na Mpango Kazi wa Kampuni wa Usalama, Afya na Mazingira Eneo la Kazi.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha maombi, ni muhimu.
- Kuzingatia kanuni za petroli na matumizi yarasilimali za ndani (Local Content) za 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji ya chini kabisa na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu wanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa **procurement@bbnjv.com; (Ukubwa wa Barua Pepe na viambatanishi MB 20 & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza) mnamo au kabla ya tarehe 5 September 2022 , Saa 12 jioni kwa saa za Tanzania,**

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji ya chini kabisa yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka:** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

217006301

UN WOMEN
United Nations Entity for Gender Equality and the Empowerment of Women

## CALL FOR PROPOSALS

The United Nations Entity for Gender Equality and the Empowerment of Women (UN Women) Tanzania is pleased to announce a Call for Proposals from organizations with a track record in human rights, women's rights and gender equality to implement creative and innovative strategies, approaches, and interventions to transform gender norms, discriminatory behaviour and practices to promote women and girls' voices, meaningful participation, leadership, and economic rights at the local level (ward, village, streets, vitongoji, e.t.c) in the selected district councils of Dar es Salaam, Coast, Lindi, Mtwara , Arusha and Singida.

The organizations should have a base and previous experience in implementing projects in the respective regions. If it's a national organization that does not have experience in the respective regions, but plans to expand its projects to the WLER Project regions building on learnings from the implantation of similar projects, it should indicate previous collaboration with other human and women's rights organizations and networks including those promoting the rights of young women and women with disabilities; and duty bearers, including local government actors and community facilitators in the respective regions to deliver on the project objectives. The organizations should also demonstrate experience working with opinion makers such as community and traditional leaders, religious leaders, male gender equality and women's empowerment champions, decision-makers, and the media.

The full Call for Proposal (CFP) may be downloaded from:

https://www.unwomen.org/en/about-us/programme-implementation/2022/08/call-for-proposals-unw-esa-tza-2022-001-transforming-gender-norms

The Call for Proposals will be open until **31st August 2022 at 23.59 hrs (EAT) (Tanzanian Time).**

**All proposal MUST be submitted through email cfp.tanzania@unwomen.org with subject line REF: CFP No. UNW-ESA-TZA-2022- 001 on Transforming Gender norms and discriminatory behaviours and practices at local levels to promote women and girls' voices, meaningful participation, and leadership.**

Only **those short listed** will be contacted for further screening and consideration.

**Proposals received after the deadline will not be considered.**

**For more information, please email: agness.hanti@unwomen.org by 31st August 2022 at 23.59 hrs (EAT)**

217003101



Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mashimba Ndaki, akizungumza na baadhi ya wakulima na wafugaji waliohudhuria mkutano wa hadhara katika Kijiji cha Tanga Wilaya ya Malinyi mkoani Morogoro, ambapo amezitaka halmashauri na mamlaka za serikali za mikoa kutekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan kutenga maeneo kwa ajili ya malisho ya mifugo pamoja na maeneo ambayo hayajatambuliwa yatambuliwe rasmi na kusajiliwa ili kuepusha migogoro ya matumizi bora ya ardhi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mtoto wa waziri aendelea kusota mahabusu polisi

**Na Maulid Mmbaga**

MSEMAJI wa Jeshi la Polisi, David Misime, amesema bado wanamshikilia mtoto wa Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene, huku wakiendelea kukusanya ushahidi kwa hatua za kisheria zaidi.

Misime alisema, kijana huyo James Simbachawene, anakabiliwa na tuhuma za makosa ya usalama barabarani na kusababisha ajali kwa kuyagonga magari mawili.

Akizungumza jana na Nipashe, msemaji huyo alisema hadi jana mchana, kijana huyo alikuwa mahabusu na wanaendelea kukamilisha ushahidi kulingana na watu walioshuhudia tukio hilo ili hatua za kisheria zichukuliwe.

"Kesho (leo) jalada litapelekwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), ili asome na kuandaa mashtaka kwa ajili ya kumfikisha mahakamani," alisema Misime.

Juzi vipande vya video fupi vilisambaa kwenye mitandao ya kijamii ikimwonyesha James akibishana na polisi wa usalama barabarani baada ya kudaiwa kusababisha ajali kwa kugonga magari mawili likiwamo Toyota Passo yenye namba za usajili T344 DKG na kujaribu kukimbia kisha akakamatwa.

Video nyingine ilionyesha kijana huyo akitoa lugha ya matusi na alipofikishwa kituo cha polisi aliendelea kutoa lugha isiyo ya kistaarabu, alipoulizwa na mmoja wa polisi kituoni alisisitiza juu ya lugha hiyo.

Pia, alionekana akisema yuko tayari kulipa kiasi chochote cha fedha na kutumia lugha isiyo ya kistaarabu dhidi ya waliolalamika kuharibiwa magari yao.

Muda mchache, ulisambaa ujumbe kwenye mitandao ya kijamii unaoelezwa ni wa Waziri Simbachawene ukisema: "Nimeona 'clip' (kipande cha video) inayozunguka kwenye mitandao ya kijamii, nakiri kuwa huyo ni kijana wangu ambaye ni mtu mzima, anajitegemea na ana familia yake."

"Nimemwagiza Mkuu wa kituo kwa sababu amekosa adabu kwa Jeshi la Polisi na ametenda kosa la usalama barabarani, ashughulikiwe bila huruma kwa mujibu wa sheria, binafsi naomba radhi sana kwa walioathirika na mkasa huo, lakini kwa Jeshi la Polisi na Watanzania wote, poleni kwa usumbufu wowote mlioupata," alisema katika sehemu ya ujumbe huo ambao ulikuwa na mchanganyiko wa herufi kubwa na rangi mkolezo.

Katika ukurasa wa Twitter mmoja wa wananchi alibandika ujumbe huo na wananchi walitoa maoni yao kuunga mkono andiko hilo:

"Waziri kaupiga mwingi, nilifikiri mara mbili nikagundua huyo ni dogo wala si kijana, kijana mwenye hela na utashi wa wadhifa wa baba yake, alitakiwa suala limalizie pale pale tena bila hata askari kufika, let us exclude Mr. Minister in this (tumwondoe waziri katika hili)."

# Serikali yatoa ufafanuzi ajira makarani wa sensa

**Na Waandishi Wetu**

SERIKALI imetoa ufafanuzi kuhusu idadi ndogo ya watu wenye ulemavu walionufaika na ajira za muda mfupi za Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika kesho nchini.

Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, Salum Kassim Ali, alibainisha jana kuwa kati ya makarani 1,658 visiwani huko, sita ni wenye ulemavu, huku akitaja sababu za idadi ndogo ni waombaji wenye ulemavu kuwa wachache, matumizi ya teknolojia na mazingira magumu ya kazi.

Akizungumza na Nipashe jana ofisini kwake, alisema: "Miundombinu siyo rafiki kwa watu wenye ulemavu, pia kazi hii ina ugumu wake hasa katika kuzifikia kaya za wananchi katika maeneo mbalimbali mjini na vijijini."

Alibainisha kuwa makarani hao 1,658 walioajiriwa kwa Unguja na Pemba, watazifikia kaya 342,400 katika maeneo 4,313 ya shehia zote 388 za Unguja na Pemba.

Baadhi ya watu wenye ulemavu waliozungumza na Nipashe, walisema wanakabiliwa na vikwazo vingi ikiwamo ajira, ambapo nafasi wanazopata ni chache licha ya kuwa na sifa za kuajiriwa.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Watu Wenye Ulemavu Wasioona Zanzibar, Fatma Chesa, alisema teknolojia imeliacha nyuma kundi hilo.

Alisema kundi kubwa la watu wenye ulemavu halina elimu ya matumizi ya vifaa vya teknolojia, ikiwamo vishikwambi kwa wasioona, ambavyo sensa ya mwaka huu vinatumika.

Katibu wa Chama cha Wenye Ulemavu wa Kusikia, Zanzibar, Abdallah Alawi, alisema wanakabiliwa na matatizo mengi ikiwamo uhaba wa wakalimani ili kupata taarifa sahihi na kwa wakati.

Jamila Borafya mwenye ulemavu wa uoni, ni miongoni mwa wakufunzi wa sensa, alisema ushiriki wa watu wenye ulemavu kwenye ajira hizo si wa kuridhisha.

Mkurugenzi wa Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu, Ussi Khamis Debe, alisema masuala ya kundi hilo yamezingatiwa kwenye sensa na wameshirikishwa vyema kulinganishwa na mwaka 2012.

Mkurugenzi huyo ambaye ana ulemavu wa ngozi, alisema kuna watu 10 wenye ulemavu ambao wamepata ajira kwa nafasi ya wakufunzi.

Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime, alisema jana kuwa wamejiandaa vyema kuhakikisha sensa inafanyika kwa usalama, utulivu na amani ili kila Mtanzania kuhesabiwa bila kikwazo.

Mjumbe wa Kamati ya Sensa Kitaifa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Dk. Selemani Jafo, aliwataka wananchi kutowabughudhi makarani wa sensa na badala yake kuwapa ushirikiano wafanikishe shughuli hiyo na hadi sasa wameridhika na maandalizi.

Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Abubakar Kunenge, aliwaonya wanaojiandaa kufanya uhalifu wakati wa sensa kwamba watashughulikiwa ipasavyo na kwamba usalama umeimarishwa.

Mkuu wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba, amewataka makarani na wasimamizi wa sensa wasifanye kazi hiyo kama namna ya kutafuta posho pekee, bali kuthamini jukumu walilopewa na nchi walifanye kwa umakini na uaminifu.

**■Imeandikwa na Julieth Mkireri (KISARAWE), Maulid Mmbaga (DAR), Rahma Suleiman (Zanzibar) na Thobias Mwanakatwe (SINGIDA)**

# Mkopo bil. 972/- kununua vifaa vya kisasa vya utafiti

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

SERIKALI inakusudia kununua vifaa vya kisasa vya utafiti baada ya kupata Dola za Kimarekani milioni 425 (Sh. bilioni 972) ikiwa ni mkopo wa miaka mitano.

Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Omary Kipanga, alisema hayo wakati akizindua Kigoda cha Oliver Tambo katika Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), mkoani hapo.

Alisema lengo la serikali ni kununua vifaa vya kutosha ili utafiti ufanyike kwa kutumia vifaa vya kisasa zaidi na kuleta mchango mkubwa ambao utasaidia nchi kupata maendeleo.

"Mpango wa serikali ni kuona tafiti zinazofanyika zinatoa mchango wa kusaidia kutatua magonjwa ya binadamu na wanyama ili kukabiliana na changamoto zinazojitokeza," alisema. Akifafanua, alisema utafiti mbalimbali unaofanyika matokeo yake yanatumika kutatua kero kwenye jamii na serikali imekuwa ikiongeza bajeti hiyo ili kukidhi mahitaji ya kitafiti.

Pia, serikali imeongeza fedha za utafiti kutoka Shilingi bilioni tatu hadi kufikia Shilingi bilioni tisa kwa mwaka wa fedha wa 2022/2023 kwa ajili ya kuendeleza sayansi, teknolojia na ubunifu utakaowezesha kusaidia kutatua changamoto mbalimbali zinazoikabili jamii.

Kadhalika, mwaka wa fedha wa 2021/2022 serikali ilitenga Shilingi bilioni tatu katika bajeti yake na kwa kutambua umuhimu wa utafiti imeongeza mara mbili zaidi kwa mwaka wa fedha 2022/2023.

Mwenyekiti wa Kigoda cha Oliver Tambo kutoka Chuo Kikuu SUA, Prof. Gerald Misinzo, alisema mpango huo umejengwa kutokana na kazi ya Oliver Tambo, kiongozi mashuhuri wa Afrika Kusini aliyebobea katika historia ya elimu ya sayansi, analiyeamini mageuzi kupitia utoaji elimu, ushirikiano na mshikamano wa mataifa barani Afrika.

Alisema mpango huo ulitangazwa mwaka 2017 katika maadhimisho ya miaka 100 ya kuzaliwa kwa kiongozi huyo ambaye aliyepambania ukombozi wa Afrika na kukiongoza Chama cha African National Congress (ANC), wakati akiwa uhamishoni nje ya nchi.

Profesa Misinzo alisema kigoda hicho kimetoa Dola milioni moja za Kimarekani (Sh. bilioni 2.3) kwa ajili ya kufanya utafiti wenye matokeo chanya utakaotatua changamoto ya magonjwa ya wanyama na binadamu.

Pia mpango huo unalenga kuikwamua Tanzania katika magonjwa yanayoathiri ufugaji wa mifugo, pia kwa afya ya binadamu na kuharakisha maono ya nchi kimaendeleo na Ajenda ya Umoja wa Afrika 2063 (Africa we want).

Alisema kuanzishwaji kwa Kigoda hicho utawezesha mabadiliko chanya katika jamii na kutimiza mpango mkakati wa Chuo Kikuu hicho kwa mwaka 2022, Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa 2025 na mkakati wa maendeleo ya dunia yanayolenga kumkwamua kila mwananchi kuwa katika maisha bora kufikia mwaka 2030.

Prof. Misinzo alisema Kigoda cha Tafiti cha Oliver Tambo kinashirikiana na Kituo cha Uchunguzi wa Magonjwa ya Kuambukiza Kusini mwa Afrika (SACIDS) (Southern African Center for Infectious Disease Surveillance) pamoja na mpango wa Afya Moja (One Health) ulioanzishwa mwaka 2008 na vyuo mbalimbali katika nchi tano wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC), ikiongozwa na SUA.

Mpango wa vigoda vya utafiti Afrika kwa mara ya kwanza ulitangazwa mwaka 2017 katika maadhimisho ya miaka 100 ya kuzaliwa kwa kiongozi huyo muhimu wa Afrika Kusini ambaye alipambania ukombozi wa Afrika na kukiongoza Chama cha ANC, akiwa uhamishoni nje ya nchi.

# TRA yawekwa mtegoni leseni kwa madereva

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

KAMANDA wa Polisi Kikosi cha Usalama Barabarani, Wilbrod Mutafungwa, amemwagiza Ofisa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), kitengo cha utoaji wa leseni kwa kushirikana na polisi kutoa leseni za udereva kwa madereva wenye sifa na vyeti vinavyotambulika kisheria.

Alisema, watakapowabaini madereva wana leseni na wamezipata kwa njia ya panya, Idara ya Ukaguzi wa Jeshi la Polisi na Ofisa ya utoaji wa leseni TRA, watawajibishwa kisheria.

Kamanda Mutafungwa alisema wamebaini madereva wengi wanaosababisha ajali nyingi wana leseni walizozipata kwa njia za udanganyifu.

Alibainisha hayo jana wakati wa Tamasha la Elimu ya Usalama Barabarani kwa watumiaji wa barabara lililofanyika kitaifa wilayani Kahama, mkoani Shinyanga katika viwanja vya kituo kidogo cha mabasi CDT kwa kushikisha viongozi mbalimbali wakiwamo wa madhehebu ya dini.

Alisema, madereva wengi wanaoendesha vyombo vya moto wana leseni bila kuwa na vyeti vinavyoonesha amesomea udereva kwenye chuo kinachotambulika na zinatolewa kwa njia za panya ilhali wahusika wanafahamu kufanya hivyo ni kwenda kinyume na sheria za usalama barabarani.

"Mahakama zetu ziendelee kutoa adhabu kubwa kwa madereva wanaofikishwa mahakamani kwa makosa ya uvunjaji wa sheria za usalama barabarani, faini zinazotolewa kwao wanaziona za kawaida hivyo lazima wafungwe ili iwe fundisho kwao," alionya Mutafungwa.

Pia, alimtaka Mkuu wa Usalama Barabarani mkoani Shinyanga, SSP Debora Lucas, kwa kushirikiana na askari wake, kufanya ukaguzi wa mabasi yote yanayobeba wanafunzi katika shule binafsi na yatakayobainika kuwa mabovu kuyatoa namba za usajili mpaka yatakaporekebishwa.

Alisema, ajali nyingi za mabasi ya wanafunzi zinatokea kwa uzembe wa madereva, ubovu wa mifumo ya breki, matairi vipara na yatayokuwa safi baada ya ukaguzi wamiliki wapate vyeti vitavyoonyesha magari yao yamekaguliwa na yako salama kubeba wanafunzi na kuagiza lifanyike kabla ya shule kufunguliwa.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama Barabarani wilayani hapo, Idsam Mapande alisema, mawakala wa mabasi ni chanzo cha ajali barabarani kwa kucheza michezo ya kubahatisha baina yao na madereva wa mabasi yanayofanya safari za mikoani kwa Sh. 500,000.

Alisema, michezo hiyo inafanyika katika magari yanayotoka kituo cha mabasi Kahama kuelekea jijini Dar es Salaam na baada ya basi kuwahi kufika kituoni dereva hulipwa Sh. 200,000 na wakala wa basi anajilipa Sh. 300,000 na kwamba bila kukemea tabia hiyo abiria watazidi kupoteza maisha.

Mapande, aliwataka abiria kutoa taarifa za mwenendo wa dereva awapo barabarani ili kuzuia ajali zinazotokea na kupoteza maisha ya watu wasiokuwa na hatia kutokana na inapotokea ajali abiria hupaza sauti kuwa mwendokasi ulikuwa mkubwa ilhali wangetoa taarifa mapema wangezuia ajali.

# Mbunge ampongeza Samia mageuzi kilimo

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

MBUNGE wa Viti Maalum Mkoa wa Dodoma, Mariam Ditopile, amempongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kutoa Sh. bilioni 150 ruzuku ya mbolea kwa ajili ya kupunguza makali ya bei ya bidhaa hiyo nchini.

Aidha, alimwomba Rais Samia akutane na wakulima wadogo, wakubwa, wawekezaji na wadau wa sekta ya kilimo ili kusikiliza ushauri na maoni yao.

Aliyasema hayo jana jijini hapo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu serikali ilivyoleta mageuzi makubwa kwenye sekta ya kilimo kwa kuongeza bajeti na kumpongeza Rais Samia kwa jambo la kihistoria la ugawaji ruzuku ya mbolea.

Alibainisha kuwa kwa sasa matumizi ya mbolea nchini yanakadiriwa kuwa kilo 19 na virutubisho kwa hekta na kwamba kiasi hicho cha matumizi ni kidogo ikilinganishwa na nchi nyingine zilizopo chini ya Jangwa la Sahara na Afrika Kusini inatumia takribani kilo 58.5 za virutubisho kwa hekta.

"Matumizi madogo ya mbolea yamekuwa yakiathiri uzalishaji na tija kwa mfano kwa zao la mahindi wastani wa uzalishaji ni tani 1.45 kwa hekta, wakati tafiti zinaonyesha nchi nyingine kama Misri ambazo zinatumia mbolea kwa wingi na kwa usahihi zinazalisha hadi kufikia tani nane za mahindi kwa hekta," alisema.

Alifafanua kuwa matumizi madogo ya mbolea nchini yanasababishwa na gharama kubwa za mbolea na uelewa mdogo wa wakulima na kutakuwa na masoko ya uhakika ya mazao.

Alisema serikali imetenga Sh. bilioni 150 kama ruzuku ili kwenda kupunguza maumivu ya bei za mbolea na kwa sasa ni vitendo na baadhi ya mikoa zoezi limeshaanza kufanyika na watu wamejitokeza kwa wingi ili kusajiliwa.







TEMBO NICKEL

## VACANCY

## EXTERNAL RELATIONS MANAGER

**Position Summary:**
Tembo Nickel is seeking to recruit an **External Relations Manager** to join the Tembo Nickel Project Team. She/he will have full responsibility to ensure the execution of the External Relations Strategy with a key focus on Environmental, Social and Governance (ESG) and maintain the company reputation. The External Relations Manager will be accountable for management of the External Relations team, internal and external communications, marketing as well as Corporate Affairs matters. The External Relations Manager will also need to work closely with Human Resources and Community Relations. This role will report to **Tembo Nickel Country Manager.**

**Duty Station: Dar es salaam Country Office with regular travel to sites**

**RESPONSIBILITIES**

- Lead on the execution of specific aspects of the Corporate Reputation Strategy - expertly managing complex external relations issues while liaising with multiple internal and external stakeholders. Create and maintain Tembo Nickel key messages for external and public dissemination.
- Day to day management of Tembo Nickel Corporate External Relations. Be the main point of contact for media and government relations.
- Develop and communicate the External Relations Strategy to key stakeholders both internally and externally. Execute Line management of External Relations team covering corporate and site team members.
- Execute communications work stream of the Environmental, Social and Governance (ESG) strategy.
- Lead on the day-to-day delivery/maintenance of Corporate publications and channels such as Tembo Nickel Newsletter as well as Tembo Nickel website and liaising with suppliers and agencies.
- Develop a strong marketing plan and brand recognition for Tembo Nickel.
- Maintain a safe and secure work environment.
- Research and implement External Relations strategic solutions.
- Develop, train and execute the roll-out of the Tembo Nickel Crisis Communications Plan.
- Maintain the organization's effectiveness and efficiency by defining and delivering strategic plans for implementing External Relations and communication.
- Complete External Relations and communication projects by coordinating resources and timetables with user departments, contractors, and other key stakeholders.
- Maintain professional and technical knowledge by attending educational workshops, reviewing professional publications, establishing personal networks, and participating in professional societies.
- Contribute to team efforts by accomplishing related results as needed.
- Actively build and manage relationships with stakeholders across media and public affairs.

**Qualifications and Competencies**

- Master's degree in public relations, communication, or related field.
- 10 years of work experience.
- Strong Corporate Relations experience either in-house or at an agency.
- Strong experience of managing communications/design/digital agencies.
- Excellent media relations skills, able to handle complex media enquiries independently.
- Strong experience of working to deliver integrated communications plans, working closely with other departments.
- Preference for experience in Crisis Communications.
- Strongly developed writing skills covering reports, internal and external communications, press releases and other publications.
- Preference for ability to translate between English and Kiswahili.

*Tembo Nickel offers a competitive remuneration package and **ONLY** shortlisted candidates will be contacted.*

**How to Apply**
Applicants are invited to send their resumes indicating the role tile in the subject via email **jobs@tembonickel.com**

**Application closing date is 30th August,2022**

**Note:** We are committed to provide equal employment opportunities based on merit and we do not charge candidates any fees in the whole recruitment process.

***Women are strongly encouraged to apply***

217005701

# MAONI & UCHAMBUZI

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Wawakilishi wetu michuano CAF msilale Kalenda ya Fifa

**WAKATI** Ligi Kuu Bara ikiwa imechezwa mizunguko miwili tu tangu ianze rasmi Agosti 15, mwaka huu, kwa sasa imeelekea mapumzikoni kupisha ratiba ya Kalenda ya Fifa ambapo wachezaji mbalimbali walioitwa kuzitumikia timu zao za taifa watajumuika nazo.

Kwa wale walioitwa katika kikosi cha timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars, walianza kujiunga nacho jana wakati huu kalenda hiyo ya Fifa ikitarajiwa kudumu hadi Septemba 04, mwaka huu.

Kwa upande wa Taifa Stars, imeingia kambini kujiandaa na mchezo wa kuwania kufuzu Fainali za Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wanaocheza Soka la Ndani (CHAN), zitakazofanyika baadaye mwaka huu nchini Algeria.

Stars inatupa karata yake ya mwisho katika kinyang'anyiro hicho kwa kuvaana nyumbani na ugenini dhidi ya Uganda kati ya Agosti 26-28 na kurudiana kati ya Septemba 2-4, mwaka huu, na timu itakayopata matokeo ya jumla katika michezo hiyo miwili, itafuzu moja kwa moja fainali hizo.

Hata hivyo, kuwapo kwa kalenda hiyo ni wazi kutakuwa kumewatibulia wawakilishi wetu wa nchi kwenye maandalizi yao michuano klabu ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika ambayo mechi za awali zinatarajiwa kupigwa kati ya Septemba 9-11 kabla ya marudiano Septemba 16-18, mwaka huu.

Ikumbukwe kwa Tanzania Bara, Simba na Yanga ndizo zinazobeba jukumu la kuiwakilisha nchi kwenye Ligi ya Mabingwa wakati Azam FC na Geita Gold FC zikibeba dhamana ya kuipeperusha vema bendera ya nchi kwenye Kombe la Shirikisho Afrika.

Hata hivyo, Azam FC yenyewe haitakuwa imeathiriwa sana na kalenda hiyo ya Fifa kutokana na ukweli kwamba itaanzia raundi ya kwanza, itakayopigwa Oktoba 7-9 na marudiano Oktoba 14-16, mwaka huu.

Hivyo, pamoja na ukweli kwamba wawakilishi wetu hao, makocha wataathirika katika programu zao za mazoezi kutokana na kuwakosa baadhi ya wachezaji, bado wanapaswa kuendelea kuwanoa watakaobaki kwa kuwa tunaamini hata wale waliopo timu za taifa wanapata mazoezi ya kutosha na kitakachokosekana ni mbinu za pamoja kama kikosi.

Hii ni kutokana na wachezaji walioitwa tu kwa upande wa Taifa Stars ni saba kutoka Klabu ya Simba, Yanga (6), Azam (5) na watatu kwa Geita Gold, idadi ambayo inaweza kuongezeka kwa klabu hizo kama wachezaji wao wa kigeni wataitwa kwenda kuzitumikia nchi zao kwenye mechi za kirafiki. Kwa mantiki hiyo, hadi kukamilika kwa Kalenda ya Fifa, zitakuwa zimebaki siku tano tu kabla ya wawakilishi hao wa nchi kimataifa kwa ngazi ya klabu, kuanza kurusha karata zao za kwanza kwa Simba kwenda nchini Malawi kuivaa Nyasa Big Bullets huku Yanga ikielekea Sudan Kusini kuvaana na Zalan FC na Geita Gold ikikwea pipa kuifuata Hilal Alsahil SC ya Sudan.

Hivyo, huu ni wakati kwa wawakilishi hao wa nchi kuendelea na maandalizi makubwa hasa ukizingatia pamoja na ligi kuanza na kuchezwa michezo miwili kwa kila timu, bado klabu hizo hazijapata muunganiko mzuri ambao unaweza kuleta matumaini ya kwenda kufanya vizuri kwenye michuano hiyo ya Afrika.


Tunataka kuona zote zikifuzu kwa kishindo kuingia raundi ya kwanza na kisha kuvuka hadi hatua ya makundi kwenye michuano hiyo yenye utajiri mkubwa kwa ngazi ya klabu Afrika, na hilo linawezekana tu kama maandalizi yataendelea kufanyika kwa umakini mkubwa.

Lakini wakati huu ambao dirisha la usajili la Ligi Kuu Bara likiwa wazi, ni wakati sahihi kwa wawakilishi wetu hao kuziba panapovuja mapema kabla ya kuelekea katika michuano hiyo migumu na yenye ushindani mkubwa.

Tunaamini katika michezo hiyo miwili ambayo kila timu imecheza kwenye Ligi Kuu, inaweza kuonyesha mapengo ambayo yanatakiwa kuzibwa mapema kabla kuingia katika kinyang'anyiro hicho cha michuano ya CAF.

Hayo yakifanyika kwa umakini mkubwa, tunaamini wawakilishi wetu wataanza michuano hiyo kwa kishindo na kujenga matarajio makubwa kwa Watanzania kushuhudia wawakilishi wetu hao wakiweka historia kwa wote kutinga hatua ya makundi, jambo ambalo tunatamani kuliona likitokea kwa mara ya kwanza kwa nchi yetu kwenye michuano hiyo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

### Waamuzi walinde wachezaji kwa rafu hizi za ovyo Ligi Kuu

Na Adam Fungamwango

**RAUNDI** ya kwanza tu ya Ligi Kuu Tanzania Bara, tayari wadau wa soka wameanza kupiga kelele kwa waamuzi kutokana na uchezaji mbaya wa baadhi ya wachezaji kwa wenzao.

Tumeona baadhi ya rafu ambazo si za kiungwana, badala yake ni zile ambazo zinaweza kumfanya kumaliza kabisa karia ya mchezaji mwenzake.

Kocha wa Yanga, Nasreddine Nabi, baada ya kumalizika kwa mechi dhidi ya Coastal Union kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid Arusha Jumamosi iliyopita, alilalamika kuhusu mwamuzi kutochukua maamuzi stahiki kwa baadhi ya matukio ambayo yalionekana ni ya kadi nyekundu.

Akasema si kwa wachezaji wa timu yake tu, bali kwa wachezaji wote wanaocheza Ligi Kuu Tanzania Bara. Nabi akasema kuna baadhi ya rafu si za kiungwana, bali ni za kuumizana, lakini waamuzi wamekuwa wakishikwa na kigugumizi kutoa maamuzi.

Analozungumza kocha huyo ni kweli kabisa. Waamuzi wa Tanzania wamekuwa hawawalindi wachezaji, badala yake wamewafanya kuwa kama wanyama ambao hawahitaji kulindwa kwa kuchezewa rafu mbaya, kusukumwa na kufanyiwa kila aina ya vitimbi bila wao kuchukua hatua.

Hii haijaanza msimu huu. Hata msimu uliopita, wachezaji wa Simba walikuwa wahanga wa rafu zisizo na kichwa wala miguu kiasi cha hadi katikati ya msimu wakawa na majeruhi zaidi ya watano.

Imefika mahali sasa wadau wa soka waanze kupaza sauti kuwaamsha waamuzi wetu ambao inaonekana mpaka mtu apasuliwe na kutokwa damu ndiyo waone ni rafu ya kadi nyekundu.

Uchunguzi wangu mdogo unaonyesha waamuzi wengi wa Tanzania ama kwa kushindwa kutafasiri sheria, woga, au kwa kutaka kusawazisha mambo wamekuwa wakizihesabu rafu badala ya kutoa adhabu kulingana na aina ya faulo yenyewe.

Kuna faulo ambayo kwa wenzetu hata ikichezwa mara moja tu, moja kwa moja ni kadi nyekundi bila kuangalia mchezaji huyo ameifanya mara ngapi na wapi, lakini huku unaweza kukuta mchezaji hata kadi ya njano hapati.

Mchezaji anataka kumvunja mwenzake mguu, anapandisha mguu kichwani, anamkata kwa nyuma, au kumsukuma, hizi zote ni rafu za kadi nyekundu tu, na wala hakuna kupepesa macho.

Hata hivyo waamuzi wetu wamekuwa waoga sana kutoa kadi ya moja kwa moja, badala yake ataanza kumhesabia alifanya mara ngapi kwa hiyo aliyoifanya ni ya mwisho.

Hii ina maana waamuzi wetu wanahesabu faulo ili watoe kadi. Ya kwanza hawatoi, ya pili anaonya, ya tatu anatoa kadi ya njano, ya nne amfuaata na kumuonyesha vidole kukumbusha ni faulo ngapi, ili mradi tu mpaka akitoa nyekundu ujue huyo mchezaji ameshindikana.

Nina uhakika, kama mwamuzi anatoka nje umpe kuchezesha Ligi ya Tanzania, anaweza kutoa kadi hata nne nyekundu kwenye mechi moja.

Unachezwa mpira kama wa mchangani kabisa na waamuzi nao wamekubaliana na hilo. Cha ajabu ni kwamba baadhi ya wachambuzi wamekuwa wakitoa video fupi kwenye baadhi ya mechi ambazo wao wanapenda kuzitoa.

Ifike wakati waamuzi sasa waanze kudili na wachezaji wakorofi ambao badala ya kuonyesha ufundi uwanjani wao wanakuwa na mikakati ya kuwaumiza wenzao.

Watu wameweka pesa kwenye ligi ili kuangalia ufundi na baadhi ya wachezaji, hivyo kukitokea wachezaji ambao hawatumii ufundi badala yake wanatumia nguvu zisizostahili waadhibiwe na waamuzi.

Na nikisema waadhibiwe si wa timu ndogo tu, hata kubwa kama za Simba, Yanga na Azam. Wakati mwingine waamuzi wamekuwa hawawachukulii hatua wachezaji wa timu ndogo kwa kucheza vibaya kwa sababu na wao wanachezewa na wachezaji wakubwa na hawaadhibiwi.

Haya yakiendelea yanaweza kusababisha maafa siku moja uwanjani, mchezaji akapoteza maisha au akapata ulemavu wa kudumu na baada ya hapo ndiyo kuanze kutolewa matamko na maagizo wakati tayari mambo yameharibika.

Nadhani waamuzi wenyewe wanajua kabisa rafu za kimpira na zisizokuwa za kiungwana, wanatakiwa watoe maamuzi sahihi bila ya kuogopa ni mchezaji wa timu gani au mashabiki. Sidhani kama kuna shabiki atalalamika kwa muda mrefu mchezaji wa upande wao atakapofanya faulo iliyostahili kadi nyekundu.

# MATANGAZO

EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

## OMBI LA KUONYESHA NIA: USIMAMIZI NA UTEKELEZAJI WA PROGRAMU YA KUREJESHA MBINU ZA KUPATA MAHITAJI YA MAISHA KUPITIA UENDELEZAJI WA UJASIRIAMALI. REJEA: 0010007865

EACOP Ltd (Kampuni) Tanzania, kampuni ya mafuta na Gesi, inaalika taasisi zenye uzoefu na sifa kuonyesha nia ya kutoa huduma ya kuandaa, kusimamia na kutekeleza ''Programu ya Kurejesha Mbinu za Kupata Mahitaji ya Maisha Kupitia Uendelezaji wa Ujasiriamali'' ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP)

Mradi wa EACOP unahusisha ujenzi na uendeshaji wa bomba litakalofukiwa chini ya ardhi litakalovuka mipaka ya nchi mbili na litakalosafirisha mafuta kutoka eneo la Ziwa Albert nchini Uganda mpaka Pwani ya Mashariki ya Tanzania kwa ajili ya kusafirisha mafuta hayo kwenda katika masoko ya Kimataifa. Bomba hili litaanzia Kabaale katika wilaya ya Hoima nchini Uganda, mpaka Chongoleani, Mkoani Tanga nchini Tanzania. Urefu wa Bomba ni kilomita 1,443, kati ya hizo, kilomita 1,147 zitakuwa Tanzania, ambapo bomba hilo litapita kwenye mikoa nane (8) ambayo ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara, na Tanga; bomba la mafuta pia litapita kwenye Halmashauri za Wilaya 27 na vijiji 231

**MAELEZO MAFUPI KUHUSU MAWANDA YA HUDUMA**

EACOP na serikali ya Tanzania wametwaa ardhi kwa ajili ya mradi. Mradi huu umeandaa Mipango Kazi ya Uhamishaji watu na Makazi (Resettlement Action Plans) kwa ajili ya vipengele tofauti tofauti au mikoa inayoguswa na mradi (zinapatikana kwenye tovuti ya EACOP: https://eacop.com/information-center/other-publications/).

Mradi upo kwenye hatua za mwisho za uandaaji wa mpango kazi wa uhamishaji watu na makazi wa ziada kwa ajili ya eneo la kituo cha kuhifadhia vifaa kilichopo baharini Tanga. Kila Mpango Kazi wa Uhamishaji wa Watu na Makazi umejumuisha mpango wa Kurejesha Mbinu za Kupata Mahitaji ya Maisha (Livelihoods Restoration Plan) na maelezo ya shughuli nane za urejeshaji wa mbinu za kupata mahitaji ya maisha Shughuli namba 7 (Uendelezaji wa Ujasiriamali) ndani ya Mpango wa Kurejesha Mbinu za Kupata Mahitaji ya

Maisha ina lengo la kusaidia kaya zilizoguswa na mradi kuweza kufanya yafuatayo:

- Kutambua fursa za kuendeleza au kukuza biashara ndogo na za kati zinazowekana kufanywa
- Kupata ujuzi wa msingi pamoja na wa hali ya juu wa Uendelezaji wa Ujasiriamali na uwezo wa kufanya kazi kwa ufanisi zaidi (haswa kwa wajasiriamali waliopo sasa na wale wenye uwezekano wa kuwa wajasiriamali baadaye, ambao huwenda hawana ujuzi wa ujasiriamali na mawazo ya biashara wakati huu)
- Kufikia fursa za masoko kwa ajili ya biashara mpya na zilizopo
- Kutambua fursa za mafunzo na ujenzi wa uwezo kwa ajili ya kaya zilizoguswa na mradi ili kuhimiza uwezo wao wa kufikia fursa za masoko
- Kutambua fursa za kupata fedha za kuwekeza kwenye biashara ndogo ndogo za kaya zilizoguswa na mradi

Walengwa wa shughuli hizi ni kaya zilizoguswa na wa Mradi wa Bomba la Mafuta la Afrika Mashariki zilizoko katika vijiji 231 na ambazo ardhi zao zilitwaliwa. Kilimo ndio mbinu tawala ya kupata mahitaji ya maisha katika maeneo yaliyoguswa na mradi. Mbinu kuu ya kaya zilizoguswa na mradi ya kupata mahitaji ya maisha ni kilimo cha kujikimu, pamoja na takribani nusu ya kaya zote kufuga mifugo, kiwango kikubwa cha wafugaji wakiwa katika mikoa kama Dodoma.

Mradi unatafuta taasisi yenye sifa na uzoefu wa kuandaa na kutekeleza programu za aina hii za uendelezaji wa ujasiriamali ili ifanye nayo kazi hizo. Taasisi itakayochaguliwa itahitajika kuwepo eneo la mradi kushirikiana moja kwa moja na wadau na na kaya zilizoguswa na mradi chini ya usimamizi na muongozo wa timu ya mradi.

**VIGEZO MUHIMU VYA KUZINGATIA:**

Taasisi zitakazoonesha nia zinaalikwa kuambatanisha maombi yao pamoja na taarifa zifuatazo:

1. Uthibitisho wa usajili kama shirika/taasisi ambayo shughuli zake zinahusiana na uendelezaji wa ujasiriamali/uboreshaji au urejeshaji wa mbinu za kupata mahitaji ya maisha ndani ya Tanzania.
2. Uthibitisho wa usajili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na cheti cha uthibitisho wa kulipa kodi kwa mwaka wa fedha uliopita.
3. Maelezo mafupi kuhusu uzoefu na uwezo wa kutekeleza programu za uendelezaji wa ujasiriamali vijijni, usimamizi wa programu kubwa za maendeleo na kufanya kazi kwa kushirikiana na sekta binafsi na serikali za mitaa. Wasilisha mifano ya kazi zinazoonyesha uzoefu wa kufanya kazi zinazofanania na hizo zilizofanywa kipindi cha karibuni, ndani miaka mitano iliyopita toka siku ya tangazo hili
4. Wafanyakazi wataopendekezwa kufanya kazi kwenye mradi huu na ujuzi na uzoefu wao katika kutekeleza programu za aina hii.
5. Inashauriwa, mwonyesha nia atume maombi ya kusajiliwa na kanzi data ya EWURA (LSSP) kama mtoaji na msambazaji wa huduma ndani ya nchi au udhibitisho kuwa wa maombi ya kusajiliwa katika kanzi data yameidhinishwa wakati wa kuwasilisha ombi la kuonyesha nia.
6. Mwombaji azingatie Kanuni ya Sekta ya Petroli ya Ushirikishwaji wa Wazawa/Ufafanuzi wa Kampuni ya Ndani

217006101

Taasisi zenye nia ya kuleta maombi na ambazo zina uwezo na rasilimali za kutekeleza shughuli au kazi zilizoorodheshwa hapo juu zinapaswa kueleza nia yao pamoja na kuambatanisha nyaraka zilizotajwa hapo juu kupitia barua pepe kwa **procurement.tz@eacop.com** (ukubwa wa barua pepe **20 Mb**) saa au kabla ya saa **11:00** saa za Afrika Mashariki (EAT) tarehe **5 Septemba 2022.** Kichwa cha Barua Pepe kiwe ni **0010007865.**

**Muhimu:** Mradi wa EACOP utapitia na kuchambua nyaraka zilizotumwa na taasisi zitakazoonyesha nia ili kutengeneza orodha ya taasisi za awali zenye vigezo vinavyotakiwa. Taasisi zitakazokidhi vigezo tu ndiyo zitapokea na kusaini Makubaliano ya Utunzaji wa Taarifa (NDA) pamoja na mwaliko wa kuwasilisha zabuni katika kuendeleza mchakato wa zabuni. Maelezo yote ya kuonyesha nia yanapaswa kuandikwa kwa lugha ya Kiingereza.

## UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
## MINISTRY OF WORKS AND TRANSPORT
## ENGINEERS REGISTRATION BOARD

## 19TH ANNUAL ENGINEERS DAY, 22nd and 23rd SEPTEMBER, 2022

## INVITATION TO PARTICIPATE TO THE EVENT

The Engineers Registration Board (ERB), a statutory body established by the Engineers Registration Act No 15 of 1997, as amended by Act No. 24 of 2007. The Board has responsibilities of regulating engineering activities and the conduct of engineers, engineering technicians and engineering consulting firms in Tanzania as well as promoting and providing opportunities and facilities for the study of and professional training in engineering.

One of the Boards functions is to organize/facilitate conferences, seminars and workshops on matters relevant to the field of Engineering.

The Board is therefore organizing an Annual Event for 19th Annual Engineers Day (AED) that will take place on **22nd and 23rd September 2022 at Dr. Jakaya Kikwete Convention Centre, Dodoma.**

The theme of the event is ***"Innovation and Skills Development in Enhancing National Sustainable Economic Development: Engineering Perspective".***

The major activities during the AED event will include:

i. Paper presentations and discussions;
ii. Feedback from the ERB Secretariat;
iii. Exhibitions of technologies, engineering goods and services;
iv. Awarding individuals, groups and firms; and
v. Oath taking for professional engineers.

The event is also a networking opportunity which also enjoys a wide media coverage.

**Engineers, engineering technicians and other stakeholders are invited to attend. 16 Professional Development Units (PDUs)** will be awarded to Engineers.

**Confirmation of participation is through payment of a registration fee as shown below:**

| Category | Participation fee | Description | Benefit |
|---|---|---|---|
| A | Tshs. 350,000/= per participant | Participants who will attend physically | • Participants will be provided with Bags and T-shirts.<br>• Practicing Engineers will be awarded 16 PDUs.<br>• Capacity building<br>• Breakfast, Refreshments, Lunch and Cocktail<br>• Networking |
| B | Tshs. 250,000/= per participant | Participants who will attend virtually with souvenir | • Participants will be provided with Bags and T-shirts.<br>• Practicing Engineers will be awarded **16** PDUs.<br>• Capacity building<br>• Video conference subscription for 2 days |
| C | Tshs. 150,000/= per participants | Participants who will attend virtually | • Practicing Engineers will be awarded 16 PDUs.<br>• Capacity building.<br>• Video conference subscription for 2 days. |

**The deadline for confirmation will be on 13th September 2022.** *Additional amount of Tshs. 50,000/= will be added to participants when payments are done after the deadline.*

All payments will be made by **control number** obtained from Annual Engineers Day online system (**www.engineersday.co.tz**). All participants are required to **first register for the event and obtain the control number,** then to pay using the invoice / control number obtained. For **group booking,** registration is through the system by opting **"bulk booking"** as well as submitting official letter with names, emails and Mobile numbers via email: **info@erb.go.tz.**

Payments for the event without a reference / Control number **will not be accepted. Online registration System opened on 16th August 2022.**

Virtual participants will be provided with Meeting ID and Password after registration through online registration system and payment of participation fee.

**Registration of Participants and collection of conference materials will be on 21st September 2022 at Dr. Jakaya Kikwete Convention Centre, Dodoma from 0900hrs.** Physical participants will be required to come with Barcode form and payment details.

Engineers are also reminded of their obligations to pay statutory fees in time and renewal of practicing licence which will become due on **1st January 2023.**

For more information on this you may contact the Board or visit Online System or scan the QR Code.

**The Registrar,**
**Engineers Registration Board,**
**P.O. Box 2768,**
**DODOMA.**
**Tel: +255-26-2960086**
**Email: registrar@erb.go.tz**
**ERB Website: www.erb.go.tz**
**Event Management System: www.engineersday.co.tz**

TANZANIA CENSUS 23 August 2022 Prepare to be Counted

216999402

# Mbunge: Msiwafiche wenye ulemavu, wazee kuhesabiwa

**Na Ashton Balaigwa,**
MOROGORO

MBUNGE wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood, amewataka wananchi kutoa ushirikiano kwa makarani wa sensa bila kuwaficha watu wenye mahitaji maalum, wakiwamo wenye ulemavu na wazee, ili kuisaidia serikali kupanga mipango ya maendeleo kulingana na idadi ya watu katika maenao husika.

Abood alitoa rai hiyo juzi baada ya kuongoza maandamano ya madereva wa bajaj na pikipiki na makundi mengine yaliyolenga kuhamasisha wananchi ndani ya jimbo hilo kujitokeza kuhesabiwa siku ya sensa.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa maandamano hayo yaliyofanyika kwenye mitaa mbalimbali ya Manispaa ya Morogoro, Abood alisema lengo la sensa ni serikali kupata idadi kamili ya Watanzania ili kuweka mipango ya maendeleo kulingana na takwimu halisi.

Alisema miongoni mwa watu ambao wanapaswa pia kuhesabiwa ni makundi ya watu maalum, wakiwamo wenye ulemavu na wazee, hivyo ni vyema wakapata nafasi hiyo kama Watanzania wengine bila kubaguliwa na jamii au familia yenye watu hao.

"Ndugu zangu tuliopo hapa leo (juzi), tumepita mitaa mbalimbali kwa ajili ya kuhamasisha watu kujitokeza katika sensa. Lengo la serikali yetu ijue idadi ya watu waliopo, ikiwamo wanawake ni wangapi, wanaume ni wangapi, watoto, wazee na watu wenye ulemavu, ili ijue uhitaji na kupanga mipango kwa wananchi kulingana na uhitaji wa eneo hilo," alifafanua.

Abood alisema ni serikali yoyote inapotaka kuweka mipango yake ya maendeleo, lazima ijue idadi ya watu wake, hivyo ni vyema wananchi wa Mkoa wa Morogoro wakatoa ushirikiano kwa maofisa wa sensa ambao watapita kila nyumba kwa ajili ya kupata takwimu hizo.

"Serikali inapoamua kupanga mahitaji kwa jamii fulani, lazima ijue idadi ya watu, hivyo niwaombe tuhesabiwe bila kuficha wenye ulemavu na wazee, ili baadaye serikali ikileta huduma, ilete kwa idadi ya watu wote," alisema.

Mwenyekiti wa Kamati ya Watu Wenye Ulemavu Mkoa wa Morogoro, Magreth Mkanga, aliwataka wazazi na walezi wa watu wenye ulemavu, kutowaficha watu wenye ulemavu wakati wa sensa hiyo iliyopangwa kuanza kesho.

Mkanga alisema matokeo ya idadi ya watu yataonyesha takwimu mbalimbali zikiwamo za kundi la watu wenye ulemavu ambazo zitasaidia katika utekelezaji wa mipango ya serikali na kamati waliyojiwekea.

Ofisa Ustawi wa Jamii Mkoa wa Morogoro, Jesca Kagunila, alisema mkoa huo kwa mwaka wa fedha 2021/22 ulitambua jumla ya watu wazima wenye ulemavu 11,415 na watoto wenye ulemavu 3,298.



Mbunge wa Morogoro Mjini, Abdulaziz Abood (mwenye miwani aliyepakiwa kwenye pikipiki), akiongoza madereva pikipiki (bodaboda) na bajaj katika mitaa mbalimbali ya Manispaa ya Morogoro kuhamasisha juzi wananchi kushiriki Sensa ya Watu na Makazi itakayoanza kesho nchini. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Kampuni yatoa gawio kwa wanahisa wake

**Na Mary Geofrey**

MKUTANO Mkuu wa Mwaka wa wanahisa wa Kampuni ya Gesi ya TOL umeidhinisha gawio la Sh. 40 kwa kila hisa.

Hatua hiyo imefikiwa baada ya kampuni hiyo kukua kwa mapato yake kwa asilimia 25 kutoka Sh. bilioni 19.8 mwaka 2020 hadi Sh. bilioni 24.8 mwaka 2021.

Mwenyekiti Bodi wa Kampuni ya TOL Gases, Michael Shirima, alitangaza gawio hilo lililopitishwa na wanahisa wote juzi jijini Dar es Salaam wakati wa mkutano huo.

Alisema faida waliyopata baada ya kulipa kodi ni asilimia 41 kutoka Sh. bilioni 2.3 kwa mwaka 2020 hadi Sh. bilioni 3.3 kwa mwaka 2021.

"Ukuaji wa mapato ya kampuni hii umechangiwa na maboresho ya kiutendaji yaliyofanyika hivi karibuni, kuwapo na mikakati ya upanuzi yaliyochangia kuimarisha nafasi ya kampuni kama mzalishaji na muuzaji wa gesi za viwandani na hospitalini.

"Kupanua wigo wa usambazaji bidhaa katika nchi nyingine za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kama vile Zambia, Zimbabwe, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo na Malawi," alisema.

Shirima alipongeza maboresho ya kiutendaji na jitihada zilizofanywa na kampuni katika kuhakikisha upatikanaji wa hewa ya oksijeni inayotumika hospitalini wakati wa mlipuko wa UVIKO-19.

"Kutokana na ugonjwa wa UVIKO-19, tulifanikisha lengo letu la kuisaidia serikali kuhakikisha upatikanaji wa gesi ya oksijeni katika kipindi kile kigumu na ninaipongeza kampuni kwa kuhakikisha upatikanaji wa gesi hiyo muhimu katika vituo mbalimbali vya huduma za afya," alisema.

Mbali na kuripoti ongezeko la faida kwa mwaka 2021, TOL Gases Limited ilielezea mikakati mbalimbali inayotarajiwa kukuza matokeo ya kifedha ya kampuni.

Alitaja moja ya mikakati hiyo ni kuzindua mradi mpya ambao ni wa pili katika Wilaya ya Rungwe na utakuza uwezo wa kampuni wa kuzalisha gesi ya ukaa.

Mwenyekiti huyo alisema mradi mpya wa gesi ya ukaa upo katika kijiji cha Ikama, wilayani Rungwe jijini Mbeya na unatarajiwa kukuza mapato ya kila mwezi kwa takribani Sh. bilioni 8.2, ikiwa ni ongezeko la asilimia 42 la mapato yatokanayo na uzalishaji wa gesi ya ukaa pekee.

# Balozi Uholanzi aona fursa kilimo viazi mviringo Tanzania

**Na Romana Mallya**

BALOZI wa Uholanzi nchini Tanzania, Wiebe de Boer, amewataka vijana wa Kitanzania kujikita kwenye kilimo cha viazi mviringo kutokana na kuwa na faida kwenye soko ndani na nje ya nchi na kubadilisha maisha yao.

Vilevile, ameitaka serikali iongeze juhudi kutafiti maeneo zaidi yanayofaa kwa kilimo hicho pamoja na kuwasaidia vijana kuanzisha mashamba makubwa ya viazi kwa maendeleo ya nchi.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati wa maadhimisho ya Siku ya Viazi Duniani, hafla iliyofanyika ubalozini humo.

Hafla hiyo ilienda sambamba na kuwatunuku vijana watatu wa kike wa Kitanzania walioshiriki shindano maalum lililoendeshwa na ubalozi huo katika mitandao ya kijamii lililopewa jina la "Potato recipe Challenge".

Mshindi wa shindano hilo ni Elice Lekasio na wengine ni Sophia Abeid na Renatha Edga, ambao walipewa zawadi mbalimbali pamoja na kutunukiwa vyeti na ubalozi huo.

Washiriki wa shindano walionyesha ubunifu wao wa kutengeneza vyakula vya aina tofauti kwa kutumia viazi aina ya Sagitta.

Balozi de Boer aliwahimiza vijana wa Kitanzania na wananchi kujikita katika kilimo cha viazi ili kujiongezea kipato.

"Ubalozi wetu tumekuwa tukiunga mkono jitihada mbalimbali za kuwasaidia wakulima hasa wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini katika kujikita katika kilimo cha mazao mbalimbali ikiwa ni pamoja na viazi na parachichi," alisema.

Alisema zao la viazi likilimwa vizuri linaweza kupata soko la ndani pamoja na nchi jirani za Kenya, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na nchi nyingine.

Alisema viazi ni mradi ambao umewezesha wakulima wengi kupata mamilioni ya shilingi nchini Uholanzi, kutokana na mbegu bora walizonazo pamoja na kuzingatia kanuni za kilimo cha kisasa.

Alisema endapo Watanzania watalipa kipaumbele zao hilo, watapata fedha nyingi na kuleta mabadiliko. Vile vile, alisema Uholanzi ina aina nyingi za mbegu za viazi ambazo zote zinastahimili magonjwa na baadhi kwa sasa zinapatikana Tanzania na kwamba ni fursa nzuri kwa vijana.

Alisema Serikali ya Uholanzi itaendelea kufanya kazi kwa karibu na Tanzania pamoja na sekta binafsi ili kusaidia utekelezaji wa mipango kadhaa ya maendeleo ikiwamo sekta ya kilimo.

Mshindi wa kwanza wa shindano hilo, Elice, alisema shindano hilo sio tu limemsaidia kuboresha ujuzi wa kutengeneza vyakula tofauti kwa kutumia viazi, bali limetoa fursa kwa watu wengi kuona umuhimu wa chakula hicho kiafya na kiuchumi.

Washindi wengine Sophia na Renatha, walionyesha ubunifu wa kutumia viazi kuandaa aina tofauti ya vyakula.

Uholanzi ni mojawapo ya nchi saba za Ulaya ambazo ziko kati ya nchi kumi za juu zinazozalisha viazi duniani. Licha ya ukweli kwamba kumekuwa na kupungua kwa uzalishaji wa viazi katika nchi nyingi za Ulaya, Uholanzi inaendelea kutumia karibu asilimia 25 ya ardhi yake kuzalisha viazi na imefanikiwa kufikia rekodi ya ulimwengu ya zaidi ya tani 45 kwa hekta.

Uholanzi inaongoza kwa mauzo ya mbegu za viazi zilizoidhinishwa duniani tani 1,000,000 kwa mwaka.

## Wakulima waitwa serikali za mitaa kupata mbolea ya ruzuku

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAKULIMA wa mikoa ya Kanda ya Ziwa wametakiwa kujitokeza katika ofisi za serikali za mitaa kwenye maeneo yao ili kujiandikisha kwa ajili ya kupata mbolea ya ruzuku.

Akizungumza na Nipashe kwa njia ya simu juzi, Kaimu Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) Kanda ya Ziwa, Hanafi Mohamed, alisema asilimia kubwa ya halmashauri katika mikoa hiyo zimepokea vitabu vya kujisajili ili kupata mbolea hiyo.

Mohamed alisema serikali imeshatoa ruzuku ya mbolea yenye thamani ya Sh. bilioni 150 ili kuwasaidia wakulima kulima kilimo chenye tija.

Pia, mamlaka hiyo kwa kanda hiyo ilikuwa inasubiri vitabu kwa ajili ya kuandikisha wakulima wenye uhitaji wa mbolea kwa shughuli za kilimo.

Alisema vitabu hivyo kwa sasa vimefika na watendaji wa kata wamepatiwa kwa ajili ya kuanza kuwasajili wakulima wote wanaohitaji mbolea.

Alisema mbolea hiyo itatolewa bure kwa kila mkulima aliyejiandikisha katika kitabu hicho kilichopo katika ofisi ya kata kwenye eneo lake.

Kuhusu namna ya kupata mbolea hiyo, alisema kila mtu ana haki ya kupata kama atakuwa anatambulika na serikali ya eneo husika.

"Vitabu vimetolewa tayari niwatake wakulima wote sasa kufika katika ofisi za kata mkiwa na vitambulisho vya mpigakura au namba ya NIDA mjiandikishe, hakuna mkulima atakayepatiwa mbolea bila kujiandikisha katika kitabu hicho," alisema.

Katika hatua nyingine, aliwataka watendaji wote wa kata katika mikoa hiyo kuhakikisha wanatoa taarifa kwa wananchi ili washiriki vyema kujisajili kunufaika na mbolea hiyo.

Katika kipindi cha kati ya mwaka 2020 na 2022, bei ya mbolea kama ya UREA kwa tani moja ilipanda kutoka Dola za Marekani 251 hadi Dola 1,214, na kuifanya serikali kutenga ruzuku ya Sh. bilioni 150 kwa ajili ya kusaidia kupunguza athari zitokanazo na mabadiliko ya bei za mbolea kwenye soko la dunia.

# 'Kila anayestahili kuhamishwa eneo uchimbaji madini kulipwa'

**Na Mwandishi Wetu,** NGARA

SERIKALI wilayani Ngara imesema italinda mradi wa uchimbaji madini wa Tembo Nickel kuhakikisha serikali na mwekezaji wananufaika.

Ofisa Tarafa ya Nyamihaga, Dadley Baham, aliyemwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Ngara, Kanali Mathias Kahabi, akizungumza kwenye kikao cha uzinduzi wa Kamati ya Kuhamasisha Watu na Makazi (RWG), kilichofanyika katika Kata ya Rulenge, alisema mradi huo ni wa kimkakati na una manufaa makubwa kwa taifa.

"Jambo kubwa hapa tunasisitiza uaminifu na uadilifu, Tembo Nickel na serikali wana ushirikiano maalum, kwa hiyo kwenye kuzuia janja janja itakuwa na jukumu la kulinda maslahi yake ndani ya mgodi huu na pia kumlinda mwekezaji.

"Msimamo wa Mkuu wa wilaya yetu ni kuwa lazima tutalinda huu mradi kwa wivu mkubwa," alisema.

Aliwataka viongozi wa vijiji na madiwani, kuwa daraja la kuelimisha wananchi mambo mbalimbali ikiwamo uthaminishaji ardhi na mali unaoendelea kwa sasa.

"Jukumu letu ni kuhakikisha mnakuwa waaminifu na daraja baina ya wananchi, mwekezaji na serikali. Nyie ndiyo mnatakiwa kutoa uelewa pale kwenye upotoshaji, mnatakiwa kutusaidia kupeleka taarifa iliyo sahihi kwa wananchi wetu. Mlio hapa ni wawakilishi ina maana mmeaminiwa na wananchi, muwapelekee taarifa sahihi.

"Sisi kazi yetu ni kuhakikisha haki inapatikana na maana ya kupata haki ni hakuna atakayeonewa," alisema.

Kwa upande wa Meneja Usalama na Afya Kazini wa Tembo Nickel, Dk. Kudra Mfaume, aliyemwakilisha Meneja Mkazi wa kampuni hiyo, Benedict Busunzu, alisema lengo lao ni kuhakikisha mgodi unaanza uzalishaji robo ya kwanza ya mwaka 2026.

Alisema pia kabla ya kuanza kwa uchimbaji, kampuni itahakikisha kila mwananchi anayehamishwa kupisha eneo la mradi anapata fidia stahiki kwa kufuata sheria za Tanzania na kanuni za kimataifa (IFC).

Alisema kuzinduliwa kwa RWG, kunatoa fursa ya majadiliano ya namna bora ya kuhamisha wananchi hao katika maeneo mengine.

Alisema uthaminishaji unaoendelea kwa sasa unafuata sheria za Tanzania na kuzingatia kanuni za kimataifa ambazo masharti yake yapo juu zaidi kwa lengo la kuhakikisha kila mwananchi anayestahili atapata fidia stahiki.

Tarehe ya ukomo ya maendelezo ya kudumu kwenye eneo la mradi wa Tembo Nickel ilitangazwa Julai 18, mwaka huu, na kwa sasa shughuli za uthaminishaji wa mali na ardhi unaendelea.

"Picha za satelaiti zilishapigwa na kuonyesha kila kitu kilicho kwenye eneo la mradi, kwahiyo ni wanaostahili tuu ambao watapata fidia sitahiki," alisema.




Meneja Usalama na Afya Kazini wa Kampuni ya Tembo Nickel, Dk. Kudra Mfaume, akizungumza wakati wa uzinduzi wa Kamati ya Uhamishaji Watu na Makazi (RWG). Kushoto ni Mwakilishi wa Mkurugenzi Wilaya ya Ngara, Solomoni Kimilike, ambaye ni Ofisa Mpango wa wilaya hiyo, Constatino Msemwa, Ofisa Tarafa ya Nyamihaga, Dadley Baham, aliyemwakilisha Mkuu wa Wilaya ya Ngara, Kanali Mathias Kahabi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadaiwa kuhujumu vibao vya anwani za makazi

**Na Gurian Adolf, SUMBAWANGA**

BAADHI ya wakazi wa mtaa wa Kasakalawe, Kata ya Katandala, Manispaa ya Sumbawanga, mkoani Rukwa wanadaiwa kuhujumu vibao vilivyoandikwa majina ya mitaa wakidai hawataki majina yaliyoandikwa kwenye vibao hivyo.

Malalamiko hayo yaliyoletwa jana kwenye mkutano wa hadhara uliofanyika kwenye mtaa huo, uliohudhuriwa na Mbunge wa Jimbo la Sumbawanga, Aesh Hillary, kwa ajili ya kusikiliza kero za wananchi na kuzipatia majibu.

Mmoja wa wakazi wa mtaa huo, Felista Mbaule, akitoa malalamiko hayo, alisema baadhi ya wananchi wanang'oa vibao vilivyokuwa vimewekwa kwa ajili ya kuonesha majina ya barabara zilizopo katika mtaa huo akidai kuwa wanaong'oa wanadai kuwa majina yaliyoandikwa hawayataki kwa kuwa hawakushirikishwa wakati wa kuyatambua.

Alisema kuwa pia wapo baadhi ya wananchi wanaong'oa vyuma hivyo wakiamini wataenda kuuza kwa wanunuzi wa vyuma chakavu hali inayo sababisha baadhi ya barabara kutokuwa na majina wakati tayari ilikuwa imekwisha bandikwa vibao na kurudisha nyuma nia ya serikali katika kutekeleza utambuzi wa anwani za makazi.

Naye Sada Hussein, alilalamikia vitendo vya kinyanyasaji vinavyofanywa na sungusungu katika kata hiyo aliyedai kuwa wanawapiga wananchi kwa kutumia nyaya hali iliyosababisha vijana wa kata hiyo kujeruhiwa kwenye miili yao na kuwa na hofu.

Awali, akitoa salamu za Chama, Katibu Mkuu wa CCM Mkoa wa Rukwa, MwanaMasood Pazi, aliwaagiza madiwani wote wanapomaliza vikao vya Baraza la Madiwani wawe wanakwenda kufanya mikutano ya hadhara na kuwapa taarifa mbalimbali wananchi.

Alisema kuwa baadhi ya maswali yanayoulizwa Mbunge yalipaswa kuwa yametolewa ufafanuzi na madiwani na kupunguza kero kupitia mabaraza ya madiwani.

Akihutubia katika mkutano huo, Mbunge Hillary aliwataka wananchi kushiriki kikamilifu sensa ya watu na makazi itakayofanyika kesho kwa kuhakikisha wanatoa ushirikiano kwa kuwapa taarifa za kweli makarani wa sensa watakapo kuwa wanatekeleza jukumu hilo.

Pia, aliwataka wakulima kwenda kwenye vijiji ambavyo wana mashamba kwa ajili ya kujiandikisha ili serikali itakapokuwa inatoa mbolea ya ruzuku wakanunue kwa bei ya ruzuku ili waweze kufanya kilimo wakiwa na uhakika wa mbolea.

Aliwaambia serikali imeamua kuweka ruzuku kwenye mbolea ili kumwezesha mkulima kuzalisha na kupata chakula kwa kuwa serikali imeamua kulipa nusu ya bei ya kwa kuchangia Sh. 70,000.

# Serikali yatoa siku 7 maandiko ya miradi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

SERIKALI imetoa siku saba kukusanywa na kuwasilishwa mkoani Dodoma maandiko ya miradi yote ya kuomba mikopo katika Mkoa wa Mwanza kutoka Benki ya Maendeleo ya Kilimo nchini (TADB) ili yafanyiwe kazi.

Agizo hilo liliitolewa mwishoni mwa wiki na Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, mkoani Mwanza alipofungua mafunzo ya vijana kuhusu ufugaji wa samaki katika Ziwa Victoria, kwa njia ya vizimba.

Vijana hao waliopata mafunzo nchini Uganda na kuhitimishwa mkoani Mwanza wanatoka katika ngazi za halmashauri.

Ulega alisema, yapo maandiko ya vikundi 10 yenye thamani ya Sh. bilioni 2.5 yaliyofikishwa TADB, lakini yamewekwa kapuni kwa zaidi ya miezi mitatu.

"Nakuagiza sasa Katibu Tawala kupeleka maandiko hayo makao makuu Dodoma siku ya Alhamisi ambayo tutakutana na wataalamu na tutamshauri waziri ili amweleweze Katibu Mkuu na sisi tutatumia mlango mwingine wa kumuona Rais moja kwa moja ili kuwasaidia watu wake kuendelea na kazi," alisema Ulega. Kadhalika, alisema Rais Samia Suluhu Hassan ameweka jumla ya Sh. bilioni 20 katika benki hiyo kwa ajili ya kuinua makundi ya vijana, wanawake na Watanzania wote wanaotaka kufanya shughuli za uzalishaji ili kulijenga taifa.

Aliwasisitiza vijana hao ambao tayari wameanza kazi hiyo na wanaotarajiwa kuanza kuwa fedha hizo zipo tayari na zinatakiwa kuingia katika uzalishaji.

Kwa upande wake, Baraka Sekadende, Mkurugenzi wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi Tanzania kituo cha Mwanza alisema serikali imetoa fedha kwa ajili ya kubainisha maeneo rafiki ya ufugaji wa samaki kwa vizimba.

"Kwa awamu ya kwanza tayari tumeainisha maeneo ya ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba katika mikoa miwili ya Kagera na Mwanza," alisema.

"Katika Mkoa wa Mwanza tumeainisha maeneo 30 ambayo yanafaa kwa ajili ya ufugaji huo," alisema.

Aliwataka vijana waliokwisha kupatiwa mafunzo ya utunzaji na ufugaji wa samaki kwa njia ya vizimba kuchangamkia fursa hiyo kwa kuwa maeneo yameainishwa na yapo tayari kwa matumizi.

# Waliovamia maeneo ya NSSF watakiwa kukubali kulipa fidia

**Na Sabina Ntobi,** TUDARCo

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amewataka wananchi waliovamia na kujenga maeneo ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), kukubali kushirikiana na Mfuko huo kulipa fidia ili wamilikishwe na kusalia maeneo hayo.

Makalla alitoa maelekezo hayo baada ya kamati iliyoundwa kuchunguza mgogoro wa wananchi waliofanya uvamizi huo na kubaini kuwa walivamia maeneo ya NSSF na kujenga kinyume na sheria.

Akizungumza na wananchi hao mwishoni mwa wiki, wakati wa ziara ya utatuzi wa migogoro ya ardhi Wilaya ya Temeke, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, ameielekeza NSSF kurasimisha upya maeneo hayo kwa kupima viwanja kwa ajili ya kulipa.

Alisema uamuzi huo ni sehemu ya busara ya serikali huku akionya tabia ya wananchi kuvamia maeneo ya watu na taasisi.

Miongoni mwa viwanja vya NSSF vilivyovamiwa na wananchi ni maeneo ya Mwapemba, Toangoma na Mtoni Kijichi na kwa eneo la Mwapemba zaidi ya wananchi 100 wamevamia eneo la NSSF lenye ukubwa wa mita za mraba 210,000 na kuweka makazi.

Kwa upande wao, baadhi ya wavamizi akiwamo, Rehema Mwita, alimshukuru Mkuu huyo wa mkoa kwa uamuzi wa kuwaruhusu kulipa fidia ili waweze kusalia katika eneo hilo na kuahidi kutoa




Ofisa Mtendaji Mkuu wa Benki ya Exim Tanzania, Jaffari Matundu (kushoto), akishirikiana na wakuu wa idara mbalimbali wa benki hiyo kuwahudumia chakula wafanyakazi wao ikiwa ni sehemu ya kusherehekea maadhimisho ya miaka 25 tangu kuanzishwa kwa benki hiyo. Hafla hiyo ilifanyika makao makuu ya benki hiyo jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadau sekta utalii wapewa mbinu kuendeleza Royal Tour

**Na Julieth Mkireri**

WAZIRI wa Maliasili na Utalii, Dk. Pindi Chana, amewataka wadau wa utalii kupokea pasi aliyoitoa Rais Samia Suluhu Hassan kwenye sekta hiyo ili kukuza utalii nchini.

Dk. Chana alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki alipokuwa akizindua mpango wa mafunzo kwa wadau katika mnyororo wa thamani uliofanyika katika Chuo cha Taifa cha Utalii.

Alisema mpango huo ni mwendelezo wa Royal Tour ambao ulizinduliwa na Rais na sekta ya utalii inaendelea kucheza na pasi ya Rais ili kuuinua katika nyanja ya kiuchumi na ajira. "Rais wetu amekuja na maono makubwa amezindua Royal Tour sasa Taifa linanufaika, haya yote ni matunda ya programu ambayo Rais ameianzisha na sasa watalii wanaendelea kuja kutokana na uongozi bora, siasa iliyopo hapa nchini kwetu," alisema.

Alipongeza chuo hicho kwa kuwa wabunifu wa kuanzisha kutoa mafunzo hayo huku akisisitiza kuendelea kubadilika kwa kubuni mbinu za kukuza utalii ambazo zitakuwa sehemu ya kuboresha sekta hiyo.

"Mpango huu umekuja katika kipindi muafaka ambapo programu ya Royal Tour imezinduliwa na Rais, na sisi tunatakiwa kucheza nafasi ya mama ametupa pasi lazima tufunge magoli, rasilimali tulizonazo nchini lazima tujue namna ya kuzitunza na kuziendeleza kwa kujiongeza na kuwa na mikakati," alisisitiza.

Alizitaka taasisi za kifedha ambazo ni sehemu ya wanufaika wa sekta hiyo kuendelea kushirikiana na sekta hiyo kufanikisha mpango huo, pia kwa kuwekeza huduma zao kwenye maeneo ya utalii huku akiipongeza benki ya NMB kwa mchango wake wa Sh. milioni 20 kufanikisha mafunzo hayo.

Dk. Chana alisema, sekta ya utalii na maliasili inachangia asilimia 25 ya fedha za kigeni na zaidi ya asilimia 17 ya Pato la Taifa, kwa upande wa ajira ni milioni 1.6 za moja kwa moja na zisizo rasmi zimepatikana.

Naye Kamishna Jenerali wa Uhamiaji nchini, Dk. Anna Makakala, alisema jeshi hilo liko tayari kupokea mafunzo hayo yatawasaidia kuimarisha utoaji huduma kwa wageni wanaoingia na kutoka nchini.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Utalii, Dk. Shogo Mlozi, alisema mafunzo hayo yataanza kutolewa kwa maofisa 700 kutoka Idara ya Uhamiaji na wengine wanaolengwa ni askari polisi, waandishi wa habari, wadau wa usafiri na watoa huduma za chakula.

Mpango huo unatarajia kuwafikia wadau 5,000 walioko kwenye mnyororo wa utalii na kuwezesha kukuza sekta hiyo hadi kufikia watalii milioni tano kwa mwaka ifikapo 2025.

Nipashe Spotika



WANASOKA 7 WENYE NDEGE KALI BINAFSI UK. 12-13



# WATANO AMBAO HAWAKUSTAHILI KUWANIA BALLON D'OR 2022

**NYON,** Uswisi

BALLON d'Or bila shaka ndio tuzo ya mtu binafsi yenye hadhi kubwa zaidi katika ulimwengu wa soka. Ni wale bora zaidi tu katika soka ndio ambao wamepata fursa ya kuzungusha mikono yao kwenye tuzo hiyo na kuibeba nyumbani. Tuzo ya Ballon d'Or inatolewa kwa mwanasoka anayefanya vizuri zaidi katika mwaka wa kalenda na Jarida la Habari la Ufaransa la France Football.

Tayari wametoa orodha ya wachezaji 30 watakaowania tuzo ya Ballon d'Or 2022 na wachezaji wafuatao wamejumuishwa; Karim Benzema, Trent Alexander-Arnold, João Cancelo, Casemiro, Thibaut Courtois, Ronaldo, Kevin de Bruyne, Luis Díaz, Fabinho, Phil Foden, Erling Haaland, Sébastien Haller, Harry Kane, Joshua Kimmich, Rafael Leão, Robert Lewandowski na Riyad Mahrez.

Wengine ni pamoja na Mike Maignan, Sadio Mané, Kylian Mbappé, Luka Modrić Christopher Nkunku, Darwin Núñez, Antonio Rüdiger, Mohamed Salah, Bernardo Silva, Son Heung-min, Virgil van Dijk, Vinícius Júnior na Dušan Vlahović

Lakini pamoja na kutajwa kwa majina ya wachezaji hao, kuna ambao ni wazi kabisa kwamba, hawakustahili kuwa kwenye orodha hii, makala haya inakuchambulia wachezaji watano ambao hawakustahili ambao ni hawa hapa...

**#5. Luis Diaz (Colombia/Liverpool)**

Luis Diaz alikuwa na msimu wa kuvutia. Alifanya kazi nzuri sana kwa FC Porto katika kipindi cha kwanza cha msimu wake kabla ya kukamilisha uhamisho wa kwenda Liverpool Januari. Alishinda Kombe la FA na Kombe la Carabao akiwa na 'Wekundu' hao, lakini hakucheza jukumu kubwa katika ushindi wowote.

Alitoa asisti mbili pekee katika mechi nane kwenye michuano yote miwili msimu uliopita. Diaz pia alishindwa kuiwezesha Colombia kufuzu Kombe la Dunia. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25, bila shaka ni fowadi mahiri lakini huenda hajafanya vya kutosha kupata nafasi kwenye orodha ya wachezaji 30 wanaowania Ballon d'Or.

Alimaliza msimu wa 2021-22 akiwa na mabao 22 na asisti 11 katika mechi 54 kwenye mashindano yote akiwa na Porto na Liverpool.

**#4. Joshua Kimmich (Ujerumani/Bayern Munich)**

Joshua Kimmich alifanya kazi nzuri sana kwa Bayern Munich katika safu ya kati msimu uliopita. Lakini alikosa sehemu nzuri ya msimu wa 2021-22 kutokana na majeraha. Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani, alicheza jumla ya mechi 39 katika mashindano yote akiwa na 'Bavaria' hao, akifunga mabao matatu na kutoa asisti 12.

Lakini ni jambo la kushangaza kuona kwamba, Kimmich alifanikiwa kuingia kwenye orodha fupi mbele ya mtu kama Thomas Muller, ambaye bila shaka alikuwa na ushawishi mkubwa katika ushindi wa Bayern wa Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga. Muller alifunga mabao 13 na kutoa pasi nyingi za mabao 25 katika mechi 45 kwenye mashindano yote kwa Bavaria hao msimu uliopita.

**#3 Cristiano Ronaldo (Ureno/Manchester United)**

Cristiano Ronaldo alikuwa na mwaka mzuri kwenye safu ya mabao. Lakini inafaa kufahamu kuwa Ureno ililazimika kwenda kwenye mchujo wa kufuzu Kombe la Dunia ili hatimaye kukata tiketi ya kucheza Qatar. Ronaldo amefanya kazi nzuri kwa Manchester United, lakini kujumuishwa kwake kwenye orodha hii kumekuja kwa mshangao.

'Mashetani Wekundu' walikuwa na msimu maarufu wa kutisha. Walimaliza msimu wa Ligi Kuu England 2021-22 wakiwa na pointi chache zaidi kuwahi kutokea (58). Ronaldo alifunga mabao 24 na kutoa asisti tatu katika mechi 38 kwenye mashindano yote akiwa na Man United msimu uliopita.

Hakushinda taji lolote, hivyo inasikitisha kwamba mtu kama Ciro Immobile, ambaye alimaliza msimu wa 2021-22 kama mfungaji bora wa Serie A, hakupewa nafasi mbele ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 37 katika orodha ya wachezaji 30 wa Ballon d'Or.

**#2 Harry Kane (England/Tottenham Hotspur)**

Harry Kane alihusishwa kwa kiwango kikubwa kuhamia Manchester City katika msimu wa majira ya joto wa 2021/22. Tottenham Hotspur ilikataa kumwachia na ni wazi Mwingereza huyo hakuwa na utulivu katika klabu hiyo katika nusu ya kwanza ya msimu. Alitatizika kufunga mabao, lakini hatimaye akarudisha kiwango chake baada ya Antonio Conte kuteuliwa kuwa kocha mpya Novemba.

Kane alichukua jukumu muhimu katika kufuzu kwa Spurs kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya. Alifunga mabao 27 na kutoa asisti 10 katika mechi 50 kwenye mashindano yote msimu wa 2021-22.

Inafaa kukumbuka kuwa mabao sita kati ya hayo yalipatikana kwenye Ligi Europa Conference. Hakuwa na msimu unaofaa kuandika kuhusu na kujumuishwa kwake katika orodha ya wachezaji 30 walioteuliwa kuwania Ballon d'Or.

**#1. Rafael Leao (Ureno/AC Milan)**

Rafael Leao alichaguliwa kuwa mchezaji bora wa Serie A kwa jukumu alilocheza katika ushindi wa AC Milan wa Scudetto msimu uliopita. Kwa mshambuliaji mchanga, alifanya kazi nzuri sana. Lakini kwa ujumla, kuna hisia kwamba uteuzi wa Leao umekuja kwa gharama ya wachezaji kadhaa ambao walifanya mengi zaidi.

Leao alifunga jumla ya mabao 14 na kutoa asisti 12 katika mechi 42 kwenye mashindano yote akiwa na 'Rossoneri' hao. Alishinda taji la Serie A, lakini wakati wachezaji kama Lionel Messi, Neymar, Ciro Immobile, Mason Mount na Thomas Muller wamepuuzwa, ni vigumu kuhalalisha kujumuishwa kwa Leao kwenye orodha ya wachezaji 30 wanaowania Ballon d'Or.

## ISIKUPITE

HADI Agosti mwaka huu Manchester City, ndiyo klabu yenye 'bili' kubwa ya mishahara kwa wiki kwa upande wa Ligi Kuu England, ikitoboka pauni milioni 355 kila wiki, inafuatiwa na Chelsea (pauni milioni 343), Manchester United ( pauni milioni 323), Liverpool (pauni milioni 314) na Arsenal (pauni milioni 244).



# WANASOKA 7 WENYE NDEGE KALI BINAFSI




Cristiano Ronaldo na mkewe, Georgina Rodriguez wakiwa ndani ya ndege yao. **PICHA: MTANDAO**



**LONDON,** England

KUWA mwanasoka wa kulipwa ni moja ya mambo magumu zaidi kukamilisha. Ni wachache waliochaguliwa wanaoifanya kuwa sehemu ya maisha yao na wachache zaidi wanaweza kufikia daraja la juu kabisa la ulimwengu wa soka la kisasa duniani.

**Wale wanaoifanikisha wanaweza kumudu uzuri wote wa ulimwengu na kuwapa wapendwa wao maisha ambayo wasingeweza kuyafikiria hapo awali.**

Kumiliki ndege binafsi na kutawala anga ni ndoto ya watu wengi duniani, lakini ni wachache tu wanaoweza kuigeuza kuwa ukweli.

Leo, tunawaangalia wachezaji wachache wenye utajiri mkubwa ambao wameweza kutimiza ndoto zao kwa kumiliki ndege binafsi, twende sasa...

### #7. Gareth Bale - Cessna Citation XLS+

Ununuzi wa pili kwa bei ghali zaidi katika historia ya Real Madrid (pauni milioni 90.9), Gareth Bale ni mmoja wa wachezaji wa Uingereza waliopambwa zaidi wakati wote.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Wales, ambaye hivi karibuni alijiunga na LA Galaxy ya Marekani, anaishi maisha ya kibinafsi lakini si mtu wa kukwepa kufurahia anasa za ulimwengu.

Bale ndiye mmiliki wa ndege ya kifahari aina ya Cessna Citation XLS+. Ndege hiyo inaweza kugharimu popote kati ya pauni milioni 5.2 na pauni milioni 7.6 na ni mojawapo ya ndege ya kifahari zaidi.

### #6. Paul Pogba - Gulfstream G280

Nyota wa zamani wa Manchester United, Paul Pogba ana moja ya ndege bora zaidi za binafsi katika ulimwengu wa soka, Gulfstream G280.

Ndege hiyo, ambayo inaweza kugharimu kati ya pauni milioni 14.64 na milioni 18.4, inaweza kubeba abiria kama kumi, na kuwapa safari ya kifahari.

Gulfstream G280, ambayo ni mojawapo ya kampuni zinazouza zaidi, ina kipimo cha urefu wa futi 66.10 na ina injini mbili aina ya Honeywell HTF7250G.

### #5. David Beckham - Bombardier Challenger 350

Kutoka kushinda yote katika ngazi ya klabu na Manchester United hadi kuwa mmoja wa watu maarufu zaidi katika historia ya mchezo huo, David Beckham amefurahia maisha yote ya juu.

Ndege yake nzuri ya Bombardier Challenger 350 ni mfano mwingine wa Beckham kushinda maishani.

Mmiliki mwenza wa Klabu ya Inter Miami amekuwa na ndege hiyo aliyoinunua kwa pauni milioni 22.33, amekuwa akiitumia kusafiri maili nyingi akiruka na kurudi kati ya Marekani na Uingereza.

Ndege hiyo, ambayo inaweza kubeba watu tisa, ina urefu wa futi 69', inaendeshwa na injini mbili za Honeywell HTF7350.

### #4. Zlatan Ibrahimovic - Cessna Citation Longitude

Zlatan Ibrahimovic ni mmoja wa wachezaji waliopambwa zaidi duniani. Anajulikana kwa mabao yake na ujasiri na mahojiano ya kuburudisha, Msweden huyo pia anajivunia kufanya makubwa.

Ndege yake binafsi ni Cessna Citation Longitude, yenye mabawa ya futi 65, inawakilisha kikamilifu roho ya mmiliki wake. Kwa makadirio yake ya thamani ya pauni milioni 24.58, Cessna Citation Longitude ni mojawapo ya ndege za gharama kubwa zinazomilikiwa na mwanasoka.

### #3. Neymar - Cessna Citation Sovereign+

Huku akipokea kitita cha pauni milioni 3.42 kwa mwezi, supastaa wa Paris Saint-Germain, Neymar ni mmoja wa wanamichezo wanaolipwa fedha nyingi zaidi duniani.

Mbrazil huyo ana ladha ya kucheza na mambo mazuri zaidi maishani, na Cessna Citation Sovereign+ yake ya pauni milioni 14.2 inaongeza sana ladha yake.

Ikumbukwe kwamba Cessna ni ndege ya pili binafsi ya Neymar. Ya kwanza ni Embraer Legacy 100, ambayo ilishikiliwa na mamlaka nchini Brazil baada ya kashfa ya kukwepa kodi mwaka 2016.

Ndege yake ya sasa inaweza kubeba abiria 12, inaendeshwa na injini mbili za Pratt & Whitney Canada PW306D.

### #2. Lionel Messi - Embraer Legacy 650P

Mshindi mara saba wa Ballon d'Or, Lionel Messi ni mmoja wa wanasoka tajiri zaidi katika historia ya mchezo huo.

Nyota huyo wa Paris Saint-Germain anapokea mshahara wa pauni milioni 2.82 kwa mwezi, kumaanisha kwamba hakuna kitu ambacho Messi hawezi kununua.

Lionel Messi alimkodisha mchezaji mwenzake wa zamani, Luis Suárez ndege yake nyingine binafsi yenye thamani ya pauni milioni 12, kusafiri hadi Uruguay kwa ajili ya kuwahi utambulisho wake katika klabu mpya ya Nacional ambayo imemsajili hivi karibuni.

Ndege binafsi ya Messi, Embraer Legacy 650P, ni mojawapo ya ndege za hali ya juu zaidi duniani na inaendeshwa na injini mbili za Rolls-Royce AE 3007A2, na inaweza kwenda kasi ya kilometa 528 kwa saa.

Ndege hiyo yenye thamani ya pauni milioni 25 ilitengenezwa kwa mara ya kwanza mwaka 2000 na ilikuwa ikitengenezwa kwa miongo miwili, hadi Agosti 2020.

### #1. Cristiano Ronaldo - Gulfstream G650

Nyota wa Manchester United, Cristiano Ronaldo ni mmoja wa wanamichezo mashuhuri zaidi duniani.

Mshindi huyo mara tano wa Ballon d'Or ana ladha ya vitu vya kupendeza zaidi na chaguo lake la ndege binafsi si jambo la kushangaza.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 37, anamiliki ndege ya Gulfstream G650, mojawapo ya ndege bora binafsi ambazo zinauzwa kwa fedha ndefu.

Kwa kitita cha pauni milioni 28, pia inatokea kuwa ndege binafsi ya bei ghali zaidi inayomilikiwa na mwanasoka.

Ndege hiyo inaendeshwa na injini mbili za Rolls-Royce BR725 A1-12 na inaweza kufikia kasi ya juu ya kilometa 610 kwa sasa. Ndege hiyo ni bora kwa safari za haraka za familia, ikiwa na uwezo wa kumeza hadi abiria 19.

Kwa kushangaza, G650 si ndege pekee ambayo inamilikiwa na Ronaldo. Nyota huyo pia ana Gulfstream G200, ambayo aliinunua kwa pauni milioni 20 mwaka 2015.

Hata hivyo, inaaminika kwamba Mreno huyo ameiuza ndege hiyo, kwani sasa anaona ni ndogo na haitoshelezi familia yake.

## Nukuu


"Nataka kushinda 'Ballon d'Or' hivi karibuni. Kama wengi, isipokuwa labda hakuna wengi wanaothubutu kukiri. Bado nina imani kuwa jambo gumu zaidi ni kushinda ya kwanza," **Mshambuliaji nyota wa Paris Saint-Germain na Ufaransa, Kylian Mbappe.**



"Kama ningekuwa katika nafasi ya Erik ten Hag wasiwasi wangu mkuu ungekuwa kupata nguvu uwanjani. Dhidi ya Liverpool, nisingemchezesha Cristiano Ronaldo na pia Marcus Rashford," **Nyota wa zamani wa Manchester United, Wayne Rooney kuelekea mchezo wa Liverpool na United leo usiku.**



"Nadhani imekuwa muda mrefu sana kwa Barcelona bila kushinda mataji, nilipojua kwa mara ya kwanza kwamba Barca walikuwa na nia ya kunileta kwenye klabu hii, wakati wote nilifikiri ulikuwa wakati muafaka kwangu na kwa klabu. Sikutaka kucheza maisha yangu yote katika ligi moja," **Mshambuliaji mpya wa klabu hiyo, Robert Lewandowski**






Kiungo wa Simba, Clatous Chama, akipiga mkwaju wa penalti uliozaa bao la tatu kwa timu yake wakati ikishinda 3-0 dhidi ya Geita Gold FC kwenye mechi yao ya kwanza ya ufunguzi wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2022/23 iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa Jumatano iliyopita. **MPIGAPICHA WETU**

# REKODI 5 KALI UFUNGUZI MECHI LIGI KUU BARA

**Na Adam Fungamwango**

LIGI Kuu Tanzania Bara msimu wa 2022/23, imeanza kwa kishindo tangu Agosti 15, mwaka huu kwa timu 16 kuanza mbio za kuusaka ubingwa pamoja na nafasi tatu za juu ambazo zitazifanya kushiriki kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa na Kombe la Shirikisho Afrika.

**Ilianza kwa Ihefu kudungwa bao 1-0 kwenye Uwanja wa Highland Estate dhidi ya Ruvu Shooting, Namungo ikalazimishwa sare ya mabao 2-2 dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Singida Big Stars ikashinda 1-0 dhidi ya Prisons mechi ikichezwa Uwanja wa Liti, Singida.**

Uwanja wa Sheikh Amri jijini Arusha, Yanga iliifumua Polisi Tanzania mabao 2-1, Dodoma Jiji ilikiona cha moto, ilipobugizwa mabao 3-1 dhidi ya Mbeya City Uwanja wa Liti Singida, Coastal Union iliichapa KMC bao 1-0 Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, Arusha, Simba ikaisasambua Geita Gold mabao 3-0 Uwanja wa Benjamin Mkapa, na Azam ikashinda mabao 2-1 dhidi ya Kagera Sugar.

Hizo zilikuwa ni mechi nane za raundi ya kwanza ambazo zilitengeneza rekodi mbalimbali.

Kwenye makala haya tumekukusanyia rekodi tano zilizowekwa baada ya mechi hizo, twende sasa...

### #1. Bao la kwanza Ligi Kuu

Straika wa Ruvu Shooting, Ally Bilal ameweka rekodi ya kufunga bao la kwanza la Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Mchezaji huyo aliyesajiliwa msimu huu akitokea JKT Tanzania, alipachika bao la kufungulia msimu dakika ya 18 kwenye mechi ya ufunguzi, ikichezwa Uwanja wa Highland Estate, Mbarali, Mbeya, dhidi ya wenyeji Ihefu.

Lilikuwa ni bao pekee kwenye mechi hiyo, wageni wakitoka na ushindi wa bao 1-0.

Msimu uliopita wa ligi, bao la kwanza la msimu lilifungwa na William Edgar wa Mbeya Kwanza ilipocheza mechi ya ufunguzi dhidi ya Mtibwa Sugar.

Straika huyo ambaye msimu huu amejiunga na Kagera Sugar alifunga bao pekee Mbeya Kwanza ikiwa ugenini ikiichapa Mtibwa Sugar bao 1-0.

### #2. Mabao 20 yavunja rekodi

Jumla ya mabao 20 yamepatikana kwenye mechi za raundi ya kwanza ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu na kuvunja rekodi ya mabao ya raundi ya msimu uliopita.

Idadi hiyo ya mabao msimu huu imeongezeka kwa asilimia 100 kwani kwenye mechi za raundi ya kwanza msimu uliopita, mabao 10 tu yalifungwa.

Mabao hayo ya msimu uliopita ambayo pia yalitokana na mechi nane tu za kwanza, yalipatikana kwa Namungo kuifunga Geita Gold 2-0, Coastal na Azam kutoka sare ya bao 1-1, Mtibwa Sugar kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Mbeya Kwanza, Dodoma Jiji ikaibamiza Ruvu Shooting 1-0, Mbeya City ikashinda 1-0 dhidi ya Prisons, Biashara United ikatoka suluhu dhidi ya Simba, Polisi Tanzania ikapata ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya KMC, na Yanga ikaidungua na Kagera Sugar 1-0.

### #3. Penalti za kumwaga

Raundi ya kwanza ya Ligi Kuu msimu huu imeweka rekodi ya kupatikana penalti nne.

Hakuna rekodi yoyote kabla ya hapo inayoonyesha kuwa zilipatikana idadi ya penalti hizo kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Hata hivyo, mbili ziliwekwa wavuni na zilizobaki zilikoswa. Namungo ndiyo timu iliyoanza kupata penalti msimu huu, lakini mpigaji wake Ibrahim Ally kwenye mechi dhidi ya Mtibwa Sugar alikosa, Fiston Mayele naye akikosa penalti ambayo Yanga ilizawadiwa kwenye mechi dhidi ya Polisi Tanzania.

Penalti mbili zilizowekwa wavuni ni zile zilizopatikana kwenye mechi kati ya Coastal Union dhidi ya KMC, Amza Moubarack raia wa Cameroon akifunga bao pekee liliolipa ushindi Coastal, na Mzambia Clatous Chama akiitendea haki penalti ya nne iliyopatikana kwenye raundi ya kwanza, akiifungia Simba katika mechi ambayo ilishinda 3-0 dhidi ya Geita Gold.

### #4. Simba yasubiri misimu minane

Simba na Yanga zote zimeweka rekodi ya kupata penalti kwenye mechi za ufunguzi, lakini 'Wekundu wa Msimbazi' wakisubiri baada ya misimu minane kupata penalti kwenye raundi ya kwanza.

Ilipata penalti yake mara ya mwisho Agosti 24, 2013 ilipocheza mechi ya ufunguzi dhidi ya Rhino ya Tabora, Uwanja wa Ali Hassan Mwinyi, ambayo iliwekwa wavuni na Jonas Mkude, timu hizo zikitoka sare ya mabao 2-2 msimu wa Ligi Kuu 2013/14.

Yanga imepata penalti kwenye mechi ya ufunguzi baada ya misimu miwili. Tofauti ni kwamba penalti hiyo iliwekwa wavuni tofauti na ya msimu huu. Alikuwa ni Kelvin Yondani aliyefunga tuta kwenye mechi ya ufunguzi msimu wa 2018/19 ilipocheza mchezo wa kwanza ya ligi dhidi ya Mtibwa Sugar Agosti 23, 2018 ikishinda mabao 2-1.

### #5. Lusajo aweka rekodi ya Mayanga

Straika wa Namungo Reliants Lusajo amefunga mabao mawili na kuifanya timu yake kutoka sare ya 2-2 dhidi ya Mtibwa Sugar kwenye mechi iliyochezwa Agosti 15 Uwanja wa Benjamin Mkapa, naye kuweka rekodi ya kufunga mabao mawili kwenye mechi ya ufunguzi Ligi Kuu msimu huu.

Msimu uliopita, rekodi hiyo iliwekwa na Mayanga wa Polisi Tanzania, alipopachika mabao mawili kwenye mechi ya ufunguzi, raundi ya kwanza ya Ligi Kuu 2021/22, Septemba 29, 2021 Uwanja wa Ushirika, Moshi mkoani Kilimanjaro, na kuipa ushindi wa mabao 2-0.

**JE, WAJUA?**



USHINDI wa mabao 3-0 dhidi ya Bournemouth juzi, Jumamosi, unamaana Arsenal sasa imeshinda mechi zake zote za mwanzo wa msimu huu wa Ligi Kuu England, hiyo ikiwa ni kwa mara ya kwanza tangu msimu wa 2004-05.





# Wastaafu wapewa mbinu za kujikwamua kiuchumi

**Na Mwandishi Wetu,** MPWAPWA

MKUU wa Wilaya ya Mpwapwa mkoani Dodoma, Josephat Maganga, amewataka wastaafu kubuni miradi mbalimbali ya ujasiriamali ili kujikwamua kiuchumi.

Maganga alitoa rai hiyo jana wilayani hapo wakati wa ufunguzi wa mafunzo kwa wastaafu kuhusu namna ya kuendeleza miradi mbalimbali ya kiuchumi yaliyoandaliwa na Benki ya CRDB.

Alisema kustaafu siyo mwisho wa maisha kwa kuwa bado wana nguvu za kufanya mambo makubwa ya ujasiriamali ili kujipatia kipato.

Meneja CRDB Tawi la Mpwapwa, Christopher Mshanga, alisema lengo la mafunzo hayo ni kuwakumbusha wastaafu kuwa wao ni hazina kubwa kwa maendeleo ya taifa.

Alisema benki hiyo itaendelea kuwapatia elimu ya mikopo kwa wastaafu na mikopo inayotolewa ina riba nafuu kwa wastaafu.

"Tunahakikisha tunaendelea kuwapatia elimu ya mikopo na kuwapatia mikopo yenye riba nafuu inayoendana nanyi kwa kuwa mmeitumikia nchi kizalendo na uadilifu mkubwa,"alisema.

Katibu Tawala wa Wilaya, Sarah Komba, aliwataka wastaafu hao kuhakikisha wanajiunga katika umoja wao.

Pia aliwaomba wastaafu hao kuhakikisha wanafikisha elimu ya umuhimu wa sensa na kujitokeza kuhesabiwa ili serikali ipate takwimu sahihi za kupanga mipango ya maendeleo kwa Watanzania.

Baadhi ya wastaafu waliohudhuria katika mafunzo hayo, akiwamo Ezekiel Sanyagi, walisema yatakuwa na chachu kubwa katika kuwawezesha kuwa na elimu ya ujasiriamali na kuondokana na vikwazo vya kiuchumi.

Sanyagi aliomba taasisi za kifedha nchini kupunguza kiwango cha riba katika mikopo inayotolewa.




Waziri wa Maendeleo ya Jamii Jinsia, Wanawake na Makundi Maalumu, Dk. Dorothy Gwajima (kushoto) na Askofu Mkuu Jimbo Kuu Katoliki Dodoma, Askofu Beatus Kinyaiya (kulia), wakitoa kitambaa ikiwa ni ishara ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa vyumba vya madarasa na maabara katika Shule ya Sekondari ya Maria De Mattias ya jijini Dodoma jana, ambapo vitagharimu Sh. bilioni 1.5, alipofika kwenye maadhimisho ya miaka 20 ya Kijiji cha Matumaini kinacholea watoto wanaotoka kwenye mazingira magumu hivi karibuni. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Bil. 3/- zatengwa ujenzi wa viwanda vya mvinyo

**Na Valentine Oforo,** DODOMA

SERIKALI imetenga Sh. bilioni tatu kwa ajili ya kutekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa viwanda vitatu vya kisasa vya kuchakata na kuhifadhi mvinyo ghafi mkoani Dodoma.

Utekelezaji wa mradi huo ni moja kati ya mikakati ya muda mrefu ya serikali katika kutatua tatizo la ukosefu wa soko la uhakika la zabibu.

Imebainishwa kuwa ujenzi wa viwanda hivyo unatarajiwa kuanza mwezi ujao na vitajengwa katika maeneo ya Chinangali II, Wilaya ya Chamwino, Mpunguzi na Hombolo jijini Dodoma.

Naibu Waziri wa Kilimo, Anthony Mavunde, akifafanua kuhusu mradi huo jana jijini hapo, alisema viwanda hivyo vitatumiwa na wakulima kwa ajili ya kuchakata zabibu zao na kuhifadhi mvinyo ghafi.

"Kwa kutumia viwanda hivi tunavyotarajia kujenga, wakulima watakuwa wanapeleka zabibu zao kwa ajili ya kuchakatwa kitaalamu na kuwa mvinyo ghafi, mvinyo ambao utahifadhiwa kitaalamu mpaka pale wateja wa kununua watakapopatikana," alisema.

Mavunde alisema ujenzi wa viwanda hivyo unatarajia kutoa suluhisho la kudumu katika kuwasaidia wakulima hao kuondokana na hasara ya zabibu zao kuoza shambani kutokana na ukosefu wa soko la uhakika.

"Pamoja na ujenzi wa viwanda hivi, pia tumeazimia kubadili mtazamo wa wakulima ili waachane na mfumo wa kuuza mikungu ya zabibu na badala yake waone umuhimu wakuuza mvinyo ghafi ambao kwa sasa ndiyo unaohitajika na wenye viwanda," alisema.

Katika jitihada zaidi za kuinua ufanisi wa sekta ya mvinyo, Naibu Waziri Mavunde alisema wizara ipo katika mchakato wa kupitia na kuboresha sera ya biashara ya mvinyo. "Lengo ni kuwashirikisha wadau muhimu kutoka sekta binafsi ili kuwavutia wawekezaji wakubwa kutoka nje ya nchi kuja na kuwekeza katika sekta ya mvinyo nchini," alisema.

Mwenyekiti wa Umoja wa Wakulima wa Zabibu Tanzania, David Mwaka, aliishukuru serikali kwa ujenzi wa viwanda hivyo vitakwomboa wakulima wa zabibu na kuboresha ufanisi katika kilimo hicho. Alisema ili kunufaika na huduma za viwanda hivyo, wakulima wanatakiwa kujiunga katika vikundi maalum vya uzalishaji na kujiunga na Chama cha Wakulima wa Zabibu (AMCOS) kilichoanzishwa kwa ajili ya kuratibu mwenendo wa soko la zabibu.

Tanzania ni nchi ya pili kwa uzalishaji wa zabibu na mvinyo barani Afrika, ikitanguliwa na Afrika Kusini. Hata hivyo, Tanzania inayo fursa ya kufanya vizuri zaidi ya Afrika Kusini kutokana na hali yake ya hewa inayoruhusu zabibu kulimwa misimu miwili kwa mwaka, ambayo haipatikani eneo lingine lolote duniani. Mbali na fursa hiyo, zabibu zinazolimwa Tanzania (Dodoma) zinatajwa kuwa na kiwango kikubwa cha sukari kinachohitajika katika utengenezaji wa mvinyo kuliko zabibu zinazolimwa maeneo mengine ya dunia.

# TFRA yaonya wanaowatoza wakulima mbolea ya ruzuku

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (TFRA) imetoa onyo kwa wanaowatoza fedha wakulima kwenye vituo vya usajili wa mbolea ya ruzuku.

Vilevile, imebainisha kuwa hadi sasa, wakulima 71,079 wameshaingizwa kwenye mfumo wa usajili wa mbolea hiyo.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkurugenzi Mtendaji wa TFRA, Dk. Stephan Ngailo, alisema wamepokea malalamiko kutoka baadhi ya mikoa ya kuwa wanawatoza wakulima fedha za kuwasajili ili waingie kwenye mfumo wa upataji mbolea hiyo licha ya serikali kuagiza utaratibu huo ufanywe bila malipo.

Aliitaja baadhi ya mikoa ambayo wamepokea malalamiko ya aina hiyo ni Iringa, Njombe na Ruvuma, akisisitiza kuwa watakaobainika kufanya hivyo, hatua kali zitachukuliwa dhidi yao.

"Ninaomba mliopewa mamlaka ya kusajili wakulima katika serikali za vijiji, msiwatoze fedha wakulima, badala yake wapeni masharti ambayo serikali imeweka ili mkulima asajiliwe kwenye mfumo," aliagiza.

Dk. Ngailo alisema kinachotakiwa kwa mkulima ili kusajiliwa ni pamoja na kuwa na shamba katika kijiji ambacho anaishi na awe mkazi wa eneo hilo anayetambulika na serikali ya kijiji na siyo vinginevyo.

"Ninasikia wengine mnawaambia mpaka wawe na kitambulisho cha suala hilo, siyo kweli. Sharti kubwa ni mkulima awe na shamba katika kijiji hicho ambalo linatambulika na serikali ya kijiji," alisema.

Mkurugenzi huyo alisema serikali imejipanga kuhakikisha wakulima wote wanapata mbolea ya ruzuku na kuwataka kuchangamikia usajili ili waingie kwenye mfumo wa kupata mbolea hiyo.





## Spika awapa msaada mabati wajasiriamali

**Na Mwandishi Wetu,** MBEYA

SPIKA wa Bunge, Dk. Tulia Ackson, kupitia taasisi yake ya Tulia Trust, ametoa msaada wa mabati kwa kikundi cha wajasiriamali wenye ulemavu wa macho ili waezeke vibanda vyao vya biashara vilivyoko katika uwanja wa zamani wa ndege.

Taasisi hiyo imetoa msaada huo kufuatia ombi maalum ambalo kikundi hicho kiliwasilisha kupitia Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, kikitoa taarifa kuwa kimeshajenga vibanda lakini havijaezekwa.

Akikabidhi mabati hayo juzi, Katibu wa mbunge huyo, Stephene Chambanenge, alisema msaada huo unalenga kulisaidia kundi hilo.

Alisema Dk. Tulia baada ya kupokea ombi hilo la watu wenye ulemavu, aliagiza uongozi wa Taasisi ya Tulia Trust kutoa mabati hayo ili kulisaidia kundi hilo la wenye ulamavu.

"Haya mabati yapo 14 na ni mbunge wenu ameyatoa, wakati wa kampeni aliahidi kushirikiana na makundi yote, hivyo baada ya kupokea ombi lenu, alituagiza tulete," alisema Chambanenge.

Aliwapongeza wajasiriamali hao kwa kuamua kuanza kujishughulisha na shughuli ndogo za kujiingizia kipato badala ya kuendelea na maisha ya utegemezi ambayo alisema siyo mazuri.

Alisema walishirikiana na ofisi ya mkuu wa wilaya kufanya tathmini ya kinachohitajika kwa ajili ya kukamilisha vibanda vya kundi hilo na wakajiridhisha kwamba mabati hayo yatatosha.

Meneja wa Taasisi ya Tulia Trust, Jacqueline Boas, alisema mbali na kukabidhi mabati hayo, taasisi hiyo pia iliwakabidhi fedha kwa ajili ya kuwalipa mafundi wa kuezeka ili vibanda hivyo vikamilike mapema na waendelee na shughuli zao.

Alisema walipewa maelekezo na ofisi ya mbunge kutoa msaada huo kwa ajili ya kulisaidia kundi hilo ambalo limeamua kuanza kujishughulisha na kazi za ujasiriamali.

Alisema taasisi hiyo inafanya kazi moja kwa moja na jamii kwa niaba ya Dk. Tulia na kwamba kundi la watu wenye ulemavu ni sehemu ya jamii ya watu wa Jiji la Mbeya ambao wanahitaji kusikilizwa na kusaidiwa pale inapobidi.

Alisema wajasiriamali hao walionufaika na msaada huo ni wawili ambao mmoja alikuwa na shida na mabati sita na mwingine nane, akifafanua kuwa kutokana na mitaji yao, wasingemudu kuyanunua.

Mmoja wa wanufaika hao, Scolastica Lazaro, aliishukuru taasisi hiyo kwa kuwasaidia mabati hayo, akisisitiza kuwa walipata ugumu kukamilisha ujenzi huo.

Alisema wao pamoja na kwamba ni watu wenye ulemavu, waliamua kufungua biashara zao ndogo ili ziwasaidie kuendesha maisha yao na familia zao na kuachana na utegemezi.

Aliwaomba wadau wengine kuwa na moyo wa kuwasaidia pale wanapokuwa na uhitaji ili wafikie malengo yao ya kujiendeleza kimaisha.



Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, akizungumza na waandishi wa habari mwishoni mwa wiki kuhusu maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika kesho nchini kote. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## Mbeya yamulika ufanisi sensa watu na makazi

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

UONGOZI wa Mkoa wa Mbeya umesema maandalizi ya sensa ya watu na makazi yameshakamilika na yameandaliwa mazingira ya kuhakikisha kazi hiyo inafanyika kwa ufanisi katika maeneo yote ya mkoa.

Mkuu wa Mkoa huo, Juma Homera, alibainisha hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu maandalizi ya kazi hiyo, akisema kila kitu kiko sawa, akiwataka wananchi kujiandaa kuhesabiwa.

Aliwataka wananchi wa mkoa huo kuhakikisha wanatoa ushirikiano kwa makarani wa sensa watakaowatembelea na kutoa takwimu sahihi kuhusu kaya zao ili kuisaidia serikali kuwa na idadi sahihi ya watu wake.

Aliwataka wasiogope kutoa takwimu za aina yoyote kwa kuwa takwimu za sensa ni kwa ajili ya kazi hiyo tu na hazitatumika kwa matumizi mengine mabaya dhidi yao.

Homera aliwataka wananchi wenye watoto wenye ulemavu, kuhakikisha wanawaficha watoto hao ili nao wahesabiwe kwa maelezo kuwa takwimu hizo ni muhimu pia kwa ajili ya kupanga mipango ya kutoa huduma kwa makundi maalum.

"Kamati za usalama za wilaya zote zimewapanga askari katika maeneo yote kwa ajili ya kuhakikisha usalama wa wananchi, mali zao na makarani wa sensa wakati wote wa kazi hii itakapokuwa inaendelea," alisema.

Homera alisema sensa itafanyika kwa utaratibu mzuri ili kuhakikisha hakuna mwananchi anayeruka wakati wa kuhesabiwa na kwamba kazi hiyo itazingatia pia makundi maalum.

Mratibu wa Sensa Mkoa wa Mbeya, John Lyakurwa, alisema wameshayatambua na kuyaainisha maeneo ya kuhesabia 7,448 ambayo ni vijiji, vitongoji na kwenye maeneo ambako makundi maalum yanapatikana. Alisema zaidi ya makarani 8,700 na wasimamizi 940 wa sensa na TEHAMA wamepatiwa mafunzo kwa ajili ya kazi hiyo na wako tayari kuifanya muda ukifika.

Alisema makarani hao watakuwa wanawahoji wakuu wa kaya maswali mbalimbali kuhusu familia zao yakiwamo yanayohusu idadi ya watoto, umri wao, hali ya ulemavu na masuala mengine yanayohusu familia hizo.

Lyakurwa alisema kuna baadhi ya maswali ambayo majibu yake yatakuwa yanafahamika, hivyo makarani hawatauliza hasa yanayomhusu mkuu wa kaya, akifafanua kuwa endapo hatakuwapo, anatakiwa kuacha taarifa zake nyumbani.

"Makundi maalum ambayo ni ya watoto wanaoishi mitaani, watu wasiokuwa na makazi maalum, wasafiri na watu wanaofanya kazi hifadhini, watahesabiwa kuanzia saa 6:00 usiku na hakuna mtu ataachwa kwenye zoezi hili," alisema Lyakurwa.

Alibainisha kuwa vifaa kwa ajili ya kazi hiyo ambavyo ni vishikwambi, vilishafanyiwa majaribio na vikaonekana viko vizuri, hivyo kazi iliyobaki ni kuanza kuhesabu watu.

Alisema wameandaliwa wataalamu wa TEHAMA kwa ajili ya kuvirekebisha vishikwambi hivyo inapotoka vitaleta shida wakati kazi ikiendelea katika maeneo mbalimbali ya kuhesabu watu.

## Wananchi wahamasishwa kujiunga huduma za bima

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

DIWANI wa Bwawani, Halmashauri ya Wilaya ya Chunya mkoani Mbeya, Saimon Mbarawata, amevichangia vijiji viwili vya kata yake bima ya dharura ambayo ni maalum kwa ajili ya kuwasafirisha wajawazito na watoto kwenda hospitalini.

Mbaravata alitoa mchango huo juzi wakati wa mkutano wa hadhara wa kutoa elimu na kuhamasisha wananchi ulioandaliwa na Shirika la Usimamizi wa Afya na Bima katika Mkoa wa Mbeya.

Bima hiyo ijulikanayo kwa jina la Bima Chapu Chapu, inaelezwa kuwa mbali na kutumika kuwasafirisha wajawazito na watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano wanapougua, pia inatumika kusafirisha maiti kutoka hospitalini mpaka nyumbani.

Mbarawata alisema aliamua kuwachangia wananchi wake wote baada ya kupata elimu kutoka kwa wataalamu wa bima hiyo na kujiridhisha kwamba ni nzuri kwa ajili ya kuokoa maisha. Alisema kata hiyo ina vitongoji vinane ambavyo kila kimoja amekichangia Sh. 220,000 na hivyo kwa vitongoji vyote alivichangia jumla ya Sh. milioni 1.7 ambazo ni kutoka mfukoni mwake.

"Walitupatia elimu nzuri sana na hivyo mimi nikaona ni vyema niwakatie wananchi wangu, walisema kwa mtu mmoja, inatakiwa kuchangia Sh. 2,500 lakini wananchi huwa ni wagumu kuelewa ndiyo maana nimeona ni vyema niwachangie tu," alifafanua.

Alisema wananchi wengi huwa ni wagumu kupokea haraka jambo lolote linaloonekana kuwa ni geni kwao na hiyo ndiyo sababu aliona awachangie ili waanze kulipia huduma hiyo mwakani.

Msimamizi wa Mradi wa Bima ya Dharura Fasta Mkoa wa Mbeya, Mwita Isaya, alisema bima hiyo inawasaidia wananchi kusafirisha wagonjwa wao kwenda mpaka katika hospitali ya wilaya na kutoa mili kutoka hospitalini mpaka nyumbani. Alisema kwa sasa serikali imeboresha huduma za afya kuanzia zahanati mpaka hospitali na hivyo wao waliamua kuanzisha bima hiyo ili kusaidia juhudi za serikali.

Alimpongeza diwani huyo kwa kuamua kuwasaidia wananchi wake bima hiyo huku akiwataka wanasiasa na viongozi wengine kuiga mfano huo wa kuwasaidia wananchi wao.

## HABARI ZANZIBAR



# Serikali: Huduma za kijamii zitatolewa wakati wa sensa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MTAKWIMU Mkuu wa Serikali Zanzibar, Salum Kassim Ali, amesema Sensa ya Watu na Makazi haitasitisha shughuli za kijamii, bali zitaendelea kutolewa kama kawaida.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake Mazizini mjini Unguja, Ali alisema kazi hiyo haitaathiri huduma za kijamii na kiuchumi, hivyo wananchi wasiwe na wasiwasi.

Alisema maandalizi ya kazi hiyo yamekamilika na hatua itakayofuata ni siku yenyewe ya sensa ambapo makarani watapita kila kaya kwa ajili ya kupata taarifa.

Mtakwimu Mkuu alisema jumla ya maeneo ya kuhesabiwa watu kwa Zanzibar ni 4,313 yatakayofikiwa katika shehia zote 388 za Unguja na Pemba yaliyotengwa wakati wa awamu ya kwanza ya utekelezaji wa kazi hiyo, sawa na asilimia 100 ya lengo.

Alisema kazi hiyo ya kuhesabiwa watu itaanza saa 6:01 usiku wa Agosti 23 kwa kukusanya taarifa za watu wote waliolala katika mipaka ya Tanzania usiku wa kuamkia siku ya sensa.

Alisema kazi hiyo itaanza katika maeneo ya makundi maalum wakiwamo wanaosafiri katika viwanja vya ndege, visiwani na kwa watu wasio na makazi maalum, wakiwamo wavuvi.

"Zoezi litaendelea kwa makarani wa sensa wataanza kukusanya taarifa za kaya kuanzia saa 12:00 asubuhi Agosti 23," alisema.

Alibainisha kuwa kutakuwa na mkesha maalum wa sensa ambao utaishia saa 4:00 usiku wa Agosti 22 ambapo kutakuwa na mambo mbalimbali kama upigaji wa fashfash na Rais Samia Suluhu Hassan atalihutubia taifa.

Mtakwimu Mkuu huyo alisema kabla ya Agosti 23, makarani wa sensa watayatambua maeneo ya kuhesabu watu na kukusanya taarifa kwa kuhoji dodoso jamii ambalo litajibiwa na kiongozi wa shehia husika ikiwamo vituo vya afya, hospitali, huduma za fedha, masoko, shule na huduma zingine za kijamii.

Alisema sensa ya mwaka huu inatarajia kuhesabu jumla ya kaya 342,400 ambapo kwa Unguja ni kaya 246,600 na kwa Pemba ni kaya 95,800.

Alisema ushiriki wa kila mtu ni muhimu ambapo takwimu zitakazopatikana zitatumika katika utoaji wa uamuzi unaohusu ustawi wao iwe kwenye huduma za kijamii, kiuchumi na mazingira wanayoishi.

"Tukiwa na takwimu bora za sensa, tutaisaidia serikali kupanga mipango ya maendelo. Kunahitajika uhamasishaji wa wadau mbalimbali kuzitumia takwimu zitakazopatikana kutokana na sensa hii katika kutunga sera na kupanga mipango ya maendeleo ya nchi yetu," alisema.




Katibu Mkuu wa Chama cha UDP, Saumu Rashid (kushoto), akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) Mjini Zanzibar jana, kuhusu sensa ambapo aliwataka wananchi na wafuasi wa chama hicho kujitokeza katika zoezi hilo. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# UDP yajitosa kuhamasisha Sensa ya Watu na Makazi

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

CHAMA cha UDP kimewataka wafuasi wake na wananchi kujitokeza kushiriki katika Sensa ya Watu na Makazi kwa ajili ya maendeleo ya taifa.

Akizungumza na waandishi wa habari jana kisiwani hapo, Katibu Mkuu wa chama hicho, Saumu Rashidi, alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kuifanya siku ya Agosti 23 kuwa ya mapumziko ili wananchi washiriki sensa bila kipingamizi.

Alisema mapumziko hayo yatatoa fursa ya kufanikiwa kwa kazi hiyo na kuwasisitiza wananchi na wanachama kutoa taarifa sahihi kwa makarani wa sensa.

Alisema katika utekelezaji wa maendeleo, lazima kuwe na takwimu sahihi na sensa ya mwaka huu ni ya kipekee kwa kuwa kwa mara ya kwanza inatekelezwa nchi ikiwa inaongozwa na Rais mwanamke.

"Mimi kama mtendaji mkuu wa chama, nipo visiwani Zanzibar kuendelea kuhamasisha sensa katika siku zilizobaki kwa sababu maendeleo hayana chama na rasilimali kubwa ya nchi ni watu, hivyo sensa ni muhimu," alifafanua.

Katibu Mkuu aliwataka wananchi kutoihusisha sensa na masula ya kisiasa na kuweka tofauti zao pembeni ili kuungana kwa kuwa tayari kuhesabiwa kwa maendeleo ya taifa.

Aliwataka wananchi kutoa ushirikiano kwa makarani wa sensa ili kuisaidia serikali katika kupanga mipango yenye tija kwa maendeleo ya wananchi.

# Makarani wa sensa watakiwa kutunza siri

**Na Mwandishi Wetu**

MKUU wa Wilaya ya Kusini, Rajab Yussuf Mkasaba, amewataka makarani wa Sensa ya Watu na Makazi kuhakikisha wanatunza siri za wananchi wanaokwenda kuwahesabu kama Sheria ya Takwimu inavyoelekeza.

Aliagiza hayo jana baada ya kushuhudia kiapo na ujazaji mkataba kwa wasimamizi maudhui, wasimamizi TEHAMA na makarani, hafla iliyofanyika katika kituo cha mafunzo ya sensa kilichoko Shule ya Sekondari Mtule, Paje.

Mkuu wa Wilaya aliwataka watendaji hao waliokula kiapo, kuhakikisha wanakwenda kutekeleza vyema majukumu yao kwa wananchi kama mafunzo yalivyowaelekeza huku wakihakikisha taarifa za wananchi zinakuwa siri kama inavyoelekeza Sheria ya Takwimu.

Aliwataka kuhakikisha wanatoa ushirikiano mzuri kwa wananchi ili kupata taarifa sahihi wanazozihitaji kwa lengo la kusaidia kutimiza malengo yaliyokusudiwa.

Sambamba na hayo, Makasaba pia aliwataka watendaji hao kuhakikisha wanatumia lugha nzuri wakati wote wa utekelezaji wa kazi hiyo kwa wananchi ili kupata taarifa wanazozitaka kwa ufanisi zaidi.

Mratibu wa Sensa ya Watu na Makazi wa Wilaya ya Kusini, Mhina Khamis Omar, aliwataka watendaji hao kufuata maelekezo na nasaha walizopewa na Mkuu wa Wilaya ili kutekeleza vyema majukumu yao sambamba na kufanikisha vyema kazi hiyo muhimu la kitaifa itakayosaidia kupanga na kupeleka maendeleo kwa wananchi.

# GDSS yapongeza Kenya kuwapa nafasi wanawake

**Na Yasmine Protace**

WANAHARAKATI wa masuala ya semina za Jinsia na Maendeleo (GDSS), wametoa maoni ya uchaguzi mkuu uliomalizika nchini Kenya mwaka huu na kupongeza idadi kubwa ya wanawake waliochaguliwa kushika nafasi mbalimbali tofauti na miaka ya nyuma.

Juma Ally mshiriki wa GDSS alisema kuwa inatakiwa vyama vya siasa vizingatie ushiriki wa wanawake katika maamuzi ikiwamo kushika nafasi za juu katika uongozi.

"Tumeona wenzetu Kenya wamezingatia Katiba na katika uchaguzi huu wanawake wengi wamechaguliwa katika nafasi mbalimbali," alisema.

Mkurugenzi Mtendaji kutoka TGNP Mtandao, Lilian Liundi alisema, vyama vya siasa vinatakiwa kuzingatia masuala ya wanawake, katika kuongeza ushiriki nafasi mbalimbali katika chaguzi.

Alisema sheria, taratibu na kanuni zifuatwe ili kuwawezesha wanawake kushiriki kugombea nafasi ngazi mbalimbali.

"Vyama vya siasa vinatakiwa kuwaangalia wanawake katika ushiriki," alisema.

Edwin Okama kutoka TGNP, alisema kuwa kunatakiwa kuwapo na tume huru ili uchaguzi uwe wa haki.

Akizungumzia kwa upande wa wanawake nchini Kenya alisema kuwa, Katiba mpya 2010 iliwabeba wanawake na kuwapa uwezo wa kugombea nafasi za udiwani na ubunge.

Vile vile, alisema mwaka 2013 alijitokeza mwanamke mmoja kugombea nafasi ya urais.

Hata hivyo, alisema 2017 hapakuwa na mwanamke aliyejitokeza kugombea nafasi ya urais. Mwaka huu, wanawake wamejitokeza kwa wingi kugombea nafasi mbalimbali, wengi walichaguliwa katika nafasi mbalimbali isipokuwa nafasi ya urais ambayo hakuna mwanamke aliyegombea.

Alisema nchini Kenya wanatambua mchango wa mwanamke, hata uuzwaji wa fomu za kugombea nafasi yoyote kwa upande wa wanawake ziliuzwa kwa bei ya chini.

"Fomu za kugombea kwa upande wa wanawake ziliuzwa bei ya chini ili kuwawezesha wanawake kujitokeza kwa wingi kushiriki," alisema.




Baadhi ya wafanyakazi wa Kampuni ya Bia ya Serengeti wakiwa pamoja baada ya kufanikiwa kufika kwenye kilele cha Mlima Kilimanjaro (Uhuru Peak) ambao ni mrefu kuliko yote Afrika ikiwa ni sehemu ya kuhamasisha utalii wa ndani na kuifikisha chapa ya Serengeti kwenye kilele cha mlima huo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Shigella akumbusha ujenzi majengo kuzingatia mahitaji wenye ulemavu

**Na Joctan Ngelly,** GEITA

MKUU wa Mkoa wa Geita, Martin Shigella, amezitaka taasisi za umma zinapojenga majengo yake kuzingatia sheria ya majengo kwa kuweka vyoo vya watu wenye ulemavu.

Shigella alitoa rai hiyo wakati akizindua duka jipya la vifaa vya ujenzi Dar Ceramic Centre mkoani hapo, jana.

"Kwa taasisi za umma ni kuzingatia pia, tunaponunua vifaa vyetu kwa ajili ya matumizi wakati mwingine tunajisahau tunanunua vyoo kama vile hatukumbuki kuna wenzetu wenye ulemavu wanahitaji aina fulani ya na vyoo hivyo vinapatikana kwenye duka la Dar Ceramica Centre kwa hiyo ni vizuri wanapojenga majengo yao wahakikishe wanaweka vyoo vya watu wenye ulemavu."

Pia, aliwatawa wananchi kutumia vifaa vya ujenzi vilivyopo kwenye duka hilo kwa kuwa ni vya kisasa na vinafaa zaidi kwa matumizi kitaifa na kimkoa.

Shigella alisisitiza kwamba serikali imejizatiti kuendelea kukaribisha na kufanya kazi na wafanyabiashara wote wa ndani na nje ya nchi ili kuwezesha kuwapatia Watanzania huduma bora za kijamii pamoja na kukuza uchumi wa taifa kwa ujumla.

Aliahidi kutoa ushirikiano wa dhati kwa wafanya biashara wote wenye nia njema ya kuja kuwekeza na kufanya biashara katika Mkoa wa Geita, kwa sababu ukaribu wa upatikanaji wa vifaa bora vya ujenzi utaleta maendeleo kwa kasi nzuri sana mkoani Geita.

Kwa upande wake, Mkuu wa Masoko na Mauzo Tanzania, Cosmas Patrick alisema duka hilo ni wasambazaji wakubwa nchini Tanzania wa vifaa vya ujenzi na vyenye ubora kutoka Hispania, Ureno, Italia, India na China kama marumaru za sakafuni na ukutani, vifaa vya bafuni na jikoni kutoka nchi mbalimbali duniani.

Patrick alisema duka hilo limekuwa kwenye biashara hiyo tangu mwaka 1995 na mpaka sasa ina mtandao mkubwa wa maduka kwenye mikoa mbalimbali nchini Tanzania ikiwamo Dar es Salaam, Dodoma, Iringa, Mbeya, Moshi, Arusha, Mwanza na sasa tawi jipya kabisa mjini Geita.

# Mwanga Hakika yawa benki ya kibiashara

**Na Joseph Mwendapole**

BENKI ya Mwanga Hakika imebadilika kutoka ya mitaji midogo hadi ya kibiashara ili kuwezesha wateja wao kupata fursa ya kupata huduma nyingi zaidi.

Mapinduzi ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA), yamewezesha benki hiyo kuwa ya biashara na yenye ushindani kwenye soko na ongezeko la mtaji.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Benki ya Mwanga Hakika, Mhandisi Ridhiwani Mringo, alisema hayo mwishoni mwa wiki kuwa lengo kuu ni kupanua wigo wa kibiashara ili kufikia malengo ya kuwa benki kubwa ndani na nje ya Tanzania.

Alisema benki ina lengo la kuimarisha ukaribu na wateja wake na kuhakikisha wanapata huduma bora na nafuu.

Alisema Benki ya Mwanga Hakika inaonekana changa, lakini ina historia ya zaidi ya miaka 20 katika utoaji wa huduma za kifedha kwa wateja wake kupitia Mwanga Community Bank iliyokuwa ikijulikana kama Wananchi Mwanga ambayo ilianzishwa mwaka 2000.

Alisema pia Benki ya Mwanga Hakika imekuwa kwa kiasi kikubwa na tukio hilo ni la kihistoria kwa miaka miwili nyuma benki tatu ziliungana ambazo ni (EFC Tanzania Microfinance Bank, Hakika Microfinance Bank na Mwanga Community Bank) zilipounganishwa na kuunda mpya iliyojulikana kama Mwanga Hakika Microfinance Bank Limited (MHB).

Pia, alisema muungano huo haukuwa wa kihistoria pekee bali na changamoto, kulikuwa na benki tatu, miundo mitatu ya uongozi, mifumo ya uendeshaji, tamaduni za kufanya kazi na makundi matatu tofauti ya wanahisa.

"Lakini bado tulipata msingi wa pamoja wa kuungana na kuunda benki moja kwa maslahi ya wadau wake wote," alisema.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Mwanga Hakika, Jagjit Singh, alisema ukubwa wa sasa wa mizania ya benki ya Mwanga Hakika, aseti ilizonazo zinathamani ya Sh. bilioni 111, ikiwa na mikopo ya thamani ya Sh. bilioni 72, Amana za wateja bilioni 71.

Aliongeza kuwa, Benki ya Mwanga Hakika imekuwa ya biashara sasa na wateja wake wategemee huduma nyingi zaidi ya zile zilizokuwa zikitolewa awali.

**Benki ya Mwanga Hakika imekuwa ya biashara sasa na wateja wake wategemee huduma nyingi zaidi ya zile zilizokuwa zikitolewa awali.**

HABARI KIMATAIFA

## Vikosi Somalia vyamaliza uvamizi uliodumu saa 30

**MOGADISHU,** Somalia

VIKOSI vya Somalia vimedai kuwashinda wanamgambo wa Al Shabaab waliovamia hoteli moja katika mji mkuu wa Mogadishu Somalia baada ya kuzingirwa kwa hoteli hiyo na mauaji kutekelezwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa na BBC jana, takriban watu 12 waliuawa katika mkasa huo uliodumu kwa saa 30, ingawa vyombo vya habari vya ndani vinaripoti kwamba idadi ya waliokufa inaweza kuwa kubwa zaidi.

Taarifa hiyo ilisema washambuliaji walitumia vilipuzi kuingia kwenye Hoteli ya Hayat ya Mogadishu mwishoni mwa wiki hii na kudhibiti kwa nguvu na kuwachukua mateka wageni usiku kucha.

Pia ilisema kwamba kundi la wapiganaji wa Kiislamu la al-Shabab limekiri kutekeleza shambulio hilo.

Ofisa ambaye jina lake halikutajwa aliliambia shirika la habari la AFP kuwa "Vikosi vya usalama vimemaliza uvamizi huo na sasa watu wenye silaha wamekufa, hatujapata kusikia milio ya risasi kutoka kwenye jengo hilo katika saa moja iliyopita," alisema.

Iliongezwa kuwa hoteli hiyo iliharibiwa kwa kiasi kikubwa kufuatia mashambulizi makali ya vikosi vya usalama usiku wa kuamkia Jumamosi, huku video zikionyesha moshi ukifuka kwenye paa la jengo hilo. **VOA**

# Ajali juu ya ajali, 16 wafariki

**GAZIANTEP,** Uturuki

AJALI mbili zilitokea sehemu moja baada ya basi moja lililowagonga watu kadhaa waliokuwa kwenye eneo la ajali ya awali katika moja ya barabara za nchini Uturuki na kusababisha vifo vya watu 16 na wengine 21 kujeruhiwa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa na BBC ajali hizo mbili zimetokea karibu na mji wa kusini wa Gaziantep jana asubuhi, na kwamba waliofariki ni pamoja na wazima moto, waokoaji na timu ya wanahabari waliokuwa wametumwa kwenda kwenye eneo ambalo ajali ya awali ilitokea, ambapo gari lilikuwa limeacha njia.

**Wakati kundi la watu likiwa kwenye eneo la ajali ya kwanza kusaidia majeruhi na waandishi kuripoti tukio hilo, ghafla basi hilo lilienda kuwavaa likateleza na kupinduka umbali wa mita 200 hadi 220.**

Ilisema wakati kundi la watu likiwa kwenye eneo la ajali ya kwanza kusaidia majeruhi na waandishi kuripoti tukio hilo, ghafla basi hilo lilienda kuwavaa likateleza na kupinduka umbali wa mita 200 hadi 220.

Gavana wa mkoa wa Gaziantep, alisema majeruhi walikimbizwa hospitali za karibu, zimamoto watatu, wafanyikazi wawili wa dharura na waandishi wa habari wawili, ambao walikuwa ni miongoni mwa waliokufa kwenye barabara kati ya Gaziantep na Nizip.

Muungano wa wanahabari wa Uturuki ulithibitisha vifo vya wanachama wake wawili, huku picha kwenye mitandao ya kijamii zilionyesha watu kadhaa wakiwa wamelala barabarani.

Pia picha kwenye shirika la habari la DHA la Uturuki zilionyesha sehemu ya nyuma ya ambulensi ikiwa imetolewa nje na vifusi vya chuma vilivyotapakaa kuizunguka.

Waziri wa Sheria Bekir Bozdag alitangaza uchunguzi kuhusu ajali hiyo, huku baadhi ya wanasiasa nchini humo wakituma salamu zao za rambirambi mtandaoni. **BBC**



Gari ya kubebea wagonjwa iliyopata ajali. **PICHA: MTANDAO**

# Dola milioni 5 za CERF zatengwa Marekani

**WASHINGTON,** Marekani

MAREKANI imetangaza kutenga dola milioni tano kutoka katika mfuko wake mkuu wa Majibu ya Dharura (CERF) ili kushughulilkia hali mbaya inayoongozeka iliyosababishwa na ghasia za magenge Haiti.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa na VOA, mashirika ya misaada ya Umoja wa Mataifa (UN) yanasema kwamba tangu mwezi Julai, takriban watu 500 wameuawa katika mapambano kati ya magenge huko Cite Soleil nchini Haiti, eneo linalotajwa kuwa ni maskini na lenye idadi kubwa ya watu katika mji mkuu, Port au Prince.

Ofisi ya UN kwa ajili ya uratibu wa masuala ya kibinadamu inakadiria kwamba takriba watu 280,000 wamekwama katika mapigano hayo.

Pia idara hiyo ilionya kuwa hali inazidi kuwa mbaya huku ghasia zikiongezeka na kuwanyima watu chakula, maji ya kunywa na huduma za afya.

Msemaji wa OCHA Jens Laerke, alisema fedha zimetolewa na CERF kuyasaidia mashirika ya kibinadamu ambayo hayana fedha za kutosha ili kujibu mahitaji ya haraka ya wahaiti.

Msemaji huyo alikiri kwamba dola milioni tano ni kiwango kidogo huku akieleza kuwa ni kiasi cha fedha muhimu sana hivi sasa.

"Ufadhili kupitia UNICEF na WFP, wenzetu watatoa chakula, maji ya kunywa, huduma za afya, afya ya akili na elimu kuwasaidia zaidi ya watu 10,000, kinachotokea mara kwa mara tunapotoa pesa kutoka CERF ni kwamba wafadhili wengine nao wanafuatia, kwa kweli, kwa ujumbe ni ishara kwamba hili ni muhimu sana katika kuokoa maisha na kuingilia kati kunahitajika hivi sasa," alisema.

UNICEF ilisema kiasi cha asilimia 20 ya watoto huko Cite Soleil walio na umri wa chini ya miaka mitano watakabiliwa na utapiamlo wa kawaida au uliokithiri.

Pia ilisema maelfu yao wako katika hatari ya kufa kwa sababu ya ghasia za magenge ambazo zinawazuia kupata huduma zinazostahili za afya na lishe.

Shirika la Mpango wa Chakula Duniani lilisema karibu nusu ya idadi ya watu nchini Haiti kiasi cha milioni 4.4 wana shida ya chakula, huku Laerke akisema kuwapatia misaada watu wengi wenye shida kuna changamoto. **VOA**

# DRC kuchunguza kisa virusi vya ebola

**KINSHASA,** DRC

SHIRIKA la Afya Ulimwenguni (WHO) limesema maofisa wa afya katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) wanachunguza kisa kinachoshukiwa kuwa cha ugonjwa wa ebola.

Kwa mujibu wa taarifa iliyochapishwa na DW, mapema mwezi uliopita, Kongo ilitangaza kumalizika kwa mlipuko wa ebola, miezi miwili baada ya virusi hivyo kuzuka tena katika jimbo la kaskazini magharibi la Equateur.

Mamlaka nchini humo zinashuku mwanamke mmoja aliyefariki Jumatatu katika jimbo la mashariki la Kivu ya Kaskazini huenda aliambukizwa virusi hivyo.

Awali, mwanamke huyo alipatiwa matibabu katika hospitali mjini Beni kwa magonjwa mengine lakini baadaye alionyesha dalili zinazofanana na virusi vya ebola.

Mkurugenzi wa WHO Kanda ya Afrika, Matshidiso Moeti (pichani), alisema katika taarifa yake jana kwamba sampuli tayari zimepelekwa maabara kwa ajili ya uchunguzi na kwamba maofisa wa afya wanashirikiana na mamlaka za ndani kuchunguza kisa hicho. **DW**



# MABINGWA KMKM KUANZA LIGI Z'BAR NA KUNDEMBA FC

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BODI ya Ligi Zanzibar (ZLB), imetangaza ratiba ya Ligi Kuu Zanzibar kwa msimu huu mpya wa 2022/23 ambayo itaanza rasmi mapema Septemba 2, mwaka huu.

**Siku hiyo ya Septemba 2, timu ya Malindi itafungua pazia la ligi hiyo dhidi ya Black Sailor, mchezo utakaopigwa Uwanja wa Amaan majira saa 10:00 alasiri huku Mabingwa watetezi, KMKM wenyewe wakitarajiwa kuanza kutetea ubingwa wao dhidi ya Kundemba FC iliyopanda daraja msimu huu, mchezo utakaopigwa Septemba 3, uwanjani hapo majira ya saa 1:00 usiku.**

Michezo mingine ya mzunguko wa kwanza itakayopigwa Septemba 3, mwaka huu ni Maafande wa Kipanga watakaribisha Zimamoto katika Uwanja wa Amaan majira ya saa 10:00 alasiri huku Septemba 4, JKU wakiivaa Uhamiaji saa 10:00 alasiri, Polisi ikishuka dimbani hapo dhidi ya Dulla Boys saa 1:00 usiku wakati Chipukizi wakiwakaribisha Mlandege katika Uwanja wa Finya Kisiwani Pemba.

Mzunguko wa kwanza utahitimishwa Septemba 5, kwa Maafande wa KVZ kuwakaribisha Maafande wenzano wa Mafunzo katika Uwanja wa Amaan saa 10:00 alasiri wakati saa 1:00 usiku Taifa Jang'ombe wakivaana na Jamhuri.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na ZLB jana, klabu zote 16 zinazoshiriki ligi hiyo, zimeshapata ratiba hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mtendaji Mkuu wa ZLB, Hashim Salum, alisema katika msimu huu kwa kuanzia hawatautumia Uwanja wa Gombani Kisiwani Pemba kwa kuwa upo katika matengenezo.

Alisema badala ya Uwanja wa Gombani klabu mbili za Ligi Kuu Zanzibar ambazo makazi yao yapo Kisiwani Pemba, zilichagua Uwanja wa Finya kuwa wao wa nyumbani katika michezo ya Ligi Kuu.

Aidha, alisema ZLB, imeridhia kila timu kupangwa uwanja waliochagua katika michezo yao ya nyumbani, lakini bodi hiyo kwa kushirikiana na kamati nyingine, watafanya ukaguzi wa viwanja hivyo na ambavyo vitahitaji maboresho wataagiza viboreshwe kwa wakati na vile ambavyo havikidhi viwango vitaondolea katika orodha ya vitakavyotumika.

"Tumetoa tayari ratiba ya mzunguko wote wa kwanza ambapo kila timu itacheza michezo 15, na kilichobaki hivi sasa tunasubiri ufunguzi wa ligi kwa mchezo wa Ngao ya Jamii ili tuanze rasmi ligi yetu," alisema.

Hata hivyo, alizitaka klabu kusoma vizuri kanuni ya mashindano ili kuhakikisha kila timu inatimiza wajibu wake kipindi ligi itakapoanza.

KIKAPU...



Vijana wakifanya mazoezi ya mpira wa kikapu katika viwanja vya Jakaya Kikwete jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Simba Queens hesabu sasa kwa AS Kigali*

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Simba Queens, Sebastian Nkoma, amesema baada ya kutinga hatua ya nusu fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika Ukanda wa Afrika Mashariki (CECAFA) kwa Wanawake, sasa anarudi uwanjani kwa ajili ya kupanga mipango mipya ya kiufundi kuhakikisha anacheza fainali ya michuano hiyo inayofanyika hapa nchini.

Simba Queens imetinga hatua ya nusu fainali baada ya kufanya vizuri na kuongoza Kundi A kwa pointi tisa, baada ya mchezo wao wa mwisho juzi, kuibuka na ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Yei Joint Stars FC ya Sudan.

Malkia wa Wekundu wa Msimbazi hao sasa watacheza nusu fainali ya kwanza dhidi ya AS Kigali ya Rwanda ambao ni wamemaliza nafasi ya pili kwenye Kundi B, mchezo huo ukitarajia kupigwa Jumatano wiki hii katika Uwanja wa Azam Complex, Chamazi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nkoma, alisema kwa sasa wanakwenda kucheza katika hatua ngumu zaidi ambayo anayefungwa anaondolewa kwenye michuano hiyo jambo ambalo anaenda kujipanga kivingine kwa ajili ya nusu fainali hiyo.

Alisema anaenda kupanga mipango ya kiufundi vizuri ili kuimarisha kikosi chake kwa kufanyia kazi mapungufu yaliyojitokeza katika michezo mitatu waliocheza hatua ya makundi.

"Tulipofikia hatua hii ni ngumu sana kwa sababu tunacheza mechi moja na ukipoteza unatoka katika mashindano, malengo yetu ni kucheza fainali na kutwaa ubingwa, hatuwezi kufika hapo hadi kupambana katika mchezo unaofuata," alisema.

Nkoma timu zote zilizovuka kwenda kucheza nusu fainali ziko vizuri na matarajio yao, mechi ijayo dhidi ya As Kigali itakuwa ya ushindani mkubwa kulinga na timu zote kuwa na vikosi bora.

"Nataka kuja na kitu kingine kabisa katika michezo iliyopo mbele yetu, hasa kutumia vizuri siku tatu za mapumziko kujifua zaidi, ili tunapocheza mechi dhidi ya AS Kigali tuonekane tofauti na mechi zilizopita," alisema Nkoma.

# Kocha wa Prisons aisikitikia Dodoma Jiji

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Msaidizi wa Prisons, Shaaban Mtupa (pichani), amesema Dodoma Jiji imerudia makosa yale yale waliyoyafanya kwenye mechi ya kwanza dhidi ya Mbeya City, hivyo nao wakayatumia kuwaadhibu.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi ya Ligi Kuu kati ya timu yake dhidi ya Dodoma Jiji katika Uwanja wa Liti, Singida juzi, Mtupa alisema Dodoma Jiji ni timu nzuri, lakini wana makosa fulani ambayo hakutaka kuyataja na lakini akaeleza ndiyo yanayowagharimu.

Mechi nzuri kwa sababu tumepata matokeo mazuri, yale mapungufu ya mechi ya kwanza tuliyafanyia kazi kwenye uwanja wa mazoezi na yametusaidia. Tuliwaangalia Dodoma Jiji kwenye mechi yao ya kwanza, kuna makosa yaliwafanya, wakapoteza, sisi tuliyajua tukayafanyia kazi, kwa bahati mbaya kwao na nzuri wameyarudia tena kwenye mechi yetu, tukayatumia na imetusaidia sisi kupata matokeo ya pointi tatu.



Ni timu nzuri, lakini bado waendelee kujipanga. Hii imeisha tunaangalia mechi inayokuja. Nina imani tutaendelea kuwa bora, ligi ndiyo kwanza inaanza, msimu huu timu yetu inaonekana ni bora zaidi kuliko msimu uliopita," alisema Mtupa, straika wa zamani wa timu hiyo.

Kocha Mkuu wa Dodoma Jiji, Mrundi Masoud Juma, alisema tatizo alilonalo ni muunganiko kwa wachezaji, huku akiahidi kuwa timu yake itakaa sawa.

"Kuanza vibaya si kusema timu ni mbaya, huu ni mwanzo wa ligi, hata timu kubwa huwa kuna wakati zinaanza vibaya, tuna wachezaji wengi wapya pamoja na kusajili vizuri. Bado kuna tatizo la muunganiko, lakini kadri muda unavyokwenda tutaanza kufanya vizuri, alisema kocha huyo

Prisons iliichapa Dodoma Jiji mabao 2-1, baada ya kutoka kuchapwa bao 1-0 dhidi ya Singida Big Stars kwenye mechi ya kwanza.

Kwa upande wa Dodoma Jiji ni mechi ya pili mfululizo kupoteza kwenye uwanja wa nyumbani, baada ya Jumatatno iliyopita kuchabangwa mabao 3-1 dhidi ya Mbeya City.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SILVA MKATABA MPYA

KIUNGO wa kati wa Manchester City, Bernardo Silva, 28, atapewa ofa ya mkataba mpya na klabu hiyo kwa nia ya kumshawishi Mreno huyo kusalia licha ya kumezewa mate na Barcelona na Paris St-Germain. ***(Star Sunday)***

### TONEY AGOMBEWA EPL

CHELSEA na Everton wameungana na Manchester United katika kupima uzito wa kumnunua mshambuliaji wa Brentford, Ivan Toney, 26. ***(Sunday Mirror)***

### TEN HAG APEWA RUHUSA

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag amepewa idhini na wamiliki wa klabu hiyo kutumia njia yake ya kutoka katika matatizo kwa kutafuta mikataba ya kuwanunua wachezaji wa Uholanzi, Frenkie de Jong, 25, kutoka Barcelona na winga wa PSV Eindhoven, Cody Gakpo, 23, pamoja na Mbrazil wa Ajax, Antony, 22. ***(Sunday Mirror)***

### PULISIC HAITAKI UNITED

MANCHESTER United wanatarajiwa kumkosa fowadi wa Chelsea, Christian Pulisic, 23, huku mchezaji huyo wa kimataifa wa Marekani akitaka kujiunga na klabu inayoshiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya ikiwa ataondoka Stamford Bridge. ***(Mail Online)***

### BELLINGHAM AWANIWA REAL

REAL Madrid itatumia fedha itakayotokana na mauzo ya Casemiro kumnunua kiungo wa kati wa Borussia Dortmund, Jude Bellingham, 19. ***(Marca)***

### SARR, ASTONI VILLA SAFI

KLABU ya Aston Villa imekubaliana ada na Watford kwa ajili ya kumnunua mshambuliaji wa Senegal, Ismaila Sarr, 24. ***(Foot Mercato via Inside Futbol)***

### PERDO AWEKWA SOKONI

MCHEZAJI Sarr Joao Pedro, 20, ndiye anayetarajiwa kunun uliwa kwa dau la pauni milioni 25 kutoka Newcastle United - huku Watford wakiwa wamekataa ofa mbili kwa mshambuliaji huyo. ***(Fabrizio Romano)***

### SPURS, LEEDS KWA GARNER

TOTTENHAM Hotspur, Leeds na Southampton zote zinamtaka kiungo wa kati wa Manchester United, James Garner, 21, licha ya Mwingereza huyo kutoanza mechi ya Ligi Kuu England. Hata hivyo, klabu zote tatu haziko tayari kulipa pauni milioni 14. ***(Sun on Sunday)***

### PICKFORD MKATABA MPYA

EVERTON imeanza mazungumzo na mlinda mlango wa England, Jordan Pickford, 28, kuhusu mkataba mpya. ***(Mail Online)***

### MUDRYK ATAKIWA ARSENAL

ARSENAL wanaangalia uwezekano wa kumnunua mshambuliaji wa Shakhtar Donetsk raia wa Ukraine, Mykhaylo Mudryk, 21. ***(Foot Media, via Sun)***

### MCTOMINAY LULU EPL

WEST Ham, Newcastle United, Everton, Leicester na Southampton zote zinavutiwa na kiungo wa kati wa Scotland na Manchester United, Scott McTominay, 25. ***(90 Min)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# ARTETA: HUYU JESUS ATAWATESA SANA TU

**LONDON,** England

KOCHA wa Arsenal, Mikel Arteta anaamini kuwa Gabriel Jesus anaweza kufikia kiwango cha juu zaidi baada ya mwanzo mzuri wa maisha yake ya soka kwenye klabu hiyo ya Kaskazini mwa Jiji la London.

**Akiwa amefunga mara mbili na kutoa pasi mbili za mabao katika ushindi wa mabao 4-2 dhidi ya Leicester wiki iliyopita, Mbrazil huyo alikuwa kwenye kiwango bora katika ushindi wa 3-0 dhidi ya Bournemouth Jumamosi, akihusika katika jukumu muhimu kwenye bao la pili la Martin Odegaard.**

Namba tisa huyo wa Arsenal hakuweza kuwa kwenye orodha ya wafungaji katika mchezo huo, baada ya lile alilofunga kukataliwa na VAR, lakini kiwango chake kilimfurahisha kocha na mashabiki wa timu hiyo.

Arteta ameonyesha kufurahishwa na mchango wa mchezaji wake huyo mpya, na anaamini bado ana nafasi ya kuboresha zaidi kiwango chake.

"Matendo yake binafsi yanaleta mabadiliko katika soka na Gabi anafanya vizuri wiki hadi wiki. Hakufunga leo, lakini alihusika kwenye mabao na mchango wake kwa timu ulikuwa wa kipekee," alisema Arteta akiiambia Sky Sports.

> ●●● Ana njaa ya kutosha na ana hamu kubwa ya kuwa bora na bora zaidi na ndicho...

"Bado ana umri wa miaka 25, hivyo anaweza kuboresha kiwango chake zaidi. Ana njaa ya kutosha na ana hamu kubwa ya kuwa bora na bora zaidi na ndicho anachohitaji kufanya."

Sifa za Arteta kwa Jesus ziliungwa mkono na nahodha wa klabu hiyo, Odegaard, aliyeelezea namna anavyofurahia kucheza na Mbrazil huyo.

"Yeye si tu anafunga mabao, anasaidia zaidi kwenye uchezaji pia, anarudi kwa kuchanganya na ana kipaji katika sehemu nyingi za mchezo. Inashangaza kucheza naye na tuna bahati sana kuwa naye hapa," alisema Odegaard.

SportPesa | LIVE IN PLAY

MECHI KALI
MANCHESTER UTD
VERSUS
LIVERPOOL

1 | 4.60
X | 4.20
2 | 1.60

PIGA *150*87#

Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# CONTE AKOSHWA NA KANE AKIFUNGA BAO LAKE LA 250



**LONDON** England

KOCHA wa Tottenham Hotspur, Antonio Conte, amemmwagia sifa mshambuliaji, Harry Kane baada ya ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Wolves, Jumamosi.

Si tu kwamba Kane alifunga bao lake la 250 kwa klabu, lakini lilikuwa ni lake la 185 kwenye Ligi Kuu England na kumchukua juu ya Sergio Aguero kwa mabao aliyofunga kwa klabu moja kwenye ligi hiyo.

Takwimu zinajieleza zenyewe na Conte alikiri kuwa hashangai tena kuona Kane akicheza nafasi hiyo muhimu kwa Spurs.


"Tunajua vema umuhimu wa Harry kwetu," alisema Conte akiiambia BBC Sport.

"Yeye ni mchezai jwa kiwango cha juu na nilifurahi sana kumuona akifunga.

"Tunazungumza kuhusu mshambuliaji wa kiwango cha kimataifa. Tunajua ustadi wake, uwezo wake, lakini wakati huo huo ni mzuri sana kufanya kazi na timu."

Baadaye katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi, Conte aliongeza: "Harry ni mchezaji ambaye anatakiwa kuleta mabadiliko, kwa ubora wake na kwa uwezo wake.

"Tunazungumza kuhusu mshambuliaji wa kiwango cha kimataifa ambaye anaweza kuwa hatari katika nyanja zote uwanjani."



## *Simeone ataka kumbakiza Griezmann*

**MADRID,** Hispania

DIEGO Simeone anatumaini, Antoine Griezmann atabakia Atletico Madrid kwa muda mrefu baada ya Mfaransa huyo kuwasaidia 'Los Colchoneros' hao kuanza vema kwenye Ligi Kuu Hispania, LaLiga.

Griezmann aliingia akitokea benchi na kufunga bao la tatu la Atletico katika ushindi mkubwa wa siku ya ufunguzi dhidi ya Getafe, Jumatatu, huku Joao Felix akiandikisha asisti tatu na Alvaro Morata akifunga mara mbili katika ushindi huo wa mabao 3-0.

Mshindi huyo wa Kombe la Dunia 2018, ana miezi 12 kwa muda wake wa mkopo wa miaka miwili katika mji mkuu wa Hispania, baada ya kuwa na kipindi kisicho na furaha akiwa na Barcelona kati ya mwaka 2019 na 2021.

Ripoti zinaonyesha Atletico wana wajibu wa kumnunua Griezmann msimu huu, na Simeone ana nia ya kumbakisha mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31.

CHEZA USHINDE KASINO

JISAJILI CHEZA SHINDA

# MTIBWA SUGAR YAIBAMIZA RUVU SHOOTING MANUNGU

**Na Adam Fungamwango**

MTIBWA Sugar imepata ushindi wake wa kwanza msimu huu ikiwa nyumbani, Uwanja wa Manungu Complex, Turiani mkoani Morogoro kwa kuichapa Ruvu Shooting mabao 2-1.

Ni ushindi wa kwanza msimu huu, kwani kwenye mechi ya kwanza ilitoka sare ya mabao 2-2 dhidi ya Namungo FC, Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Mchezaji Nassor Kuziwa, aliyepandishwa na timu hiyo kutoka kwenye kikosi cha vijana chini ya miaka 20, ndiye aliyefunga mabao yote mawili kwenye mechi hiyo.

**Alipachika mabao hayo dakika ya 22 na 56, huku bao la kufutia machozi la Ruvu Shooting, likifungwa na Abalkassim Hamisi dakika ya 46 ya mchezo.**

Ruvu Shooting ambayo kwenye mechi ya kwanza ikiwa ugenini Uwanja wa Highland Estate, Mbarali mkoani Mbeya iliichapa Ihefu FC bao 1-0, ilijitahidi kwa kila hali ikiwa na mfungaji wao, Ally Bilal, Haji Ugando na Rashid Juma kutaka kusawazisha, lakini mabeki wa wenyeji wa mechi hiyo wakiongozwa na David Kameta 'Duchu', Vedastus Mwihambi na Mkongomani Paschal Kitenge, walikaa imara kuondoa hatari zote.

Kwa matokeo hayo, Mtibwa Sugar inafikisha pointi nne, huku Ruvu Shooting ikibakiwa na alama zake tatu.

Ligi hiyo imesimama kupisha Kalenda ya Fifa hadi Septemba 6, mwaka huu, lakini Mtibwa itasuka katika dimbani lake hilo Septemba 7 kuikaribisha Ihefu FC huku Ruvu Shooting ikiifuata Namungo Septemba 11, mwaka huu.

**HAMNIWEZI...**



Beki wa kushoto wa Simba, Mohamed Hussen 'Tshabalala', akiwatoka wachezaji wa Kagera Sugar, katika mchezo wa Ligi Kuu Bara uliopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam juzi na Simba kuibuka na ushindi wa mabao 2-0. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# *Kocha wa Ihefu atoa sababu vipigo*

**Na Hadija Mngwai**

KOCHA Mkuu wa Ihefu FC, Zuberi Katwila, ametoa sababu ya kikosi chake kupoteza michezo miwili mfululizo ya Ligi Kuu Bara kwamba ni kutokana na kikosi chake kutokukaa sawa.

Ihefu iliyorejea Ligi Kuu msimu huu, imepoteza michezo miwili ya mwanzo kwa kupokea kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Ruvu Shooting na matokeo kama hayo dhidi ya Namungo FC.

Akizungumza na Nipashe jana, Katwila alisema, ligi ni ngumu na inaushindani mkubwa, hivyo lakini kupoteza michezo ya awali kwa kikosi chake ni kutokana na kutokaa sawa, lakini wanajipanga ili kufanya vema michezo inayofuata.

"Ligi ni ngumu, kuna ushindani mkubwa, tuna kikosi kizuri lakini bado hakijatupa matokeo mazuri kutokana na kutokaa sawa.

"Lakini yote kwa yote wachezaji wana jukumu la kuhakikisha wanatupatia matokeo mazuri kwa kuwa sisi tumesajili kikosi kizuri.

"Kila mchezaji anasikitika kuona tumepoteza michezo miwili mfululizo, hivyo tunajipanga katika kipindi hiki cha mapumziko ili tuweze kufanya vizuri kwenye mechi zinazofuata," alisema Katwila.

SPORTPESA APP

PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI

"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 22/08/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4362 | Ansan Greeners vs Chungnam Asan | 3.43 | 3.29 | 1.98 |
| 14:30 | 2711 | Beijing Guoan vs Guangzhou RF | 1.19 | 5.71 | 11.81 |
| 14:30 | 3263 | Meizhou Kejia vs Wuhan Three Towns FC | 10.76 | 5.48 | 1.21 |
| 17:00 | 2973 | Universitatea Cluj vs Sepsi Osk | 3.25 | 3.05 | 2.25 |
| 18:00 | 2398 | Honka vs Hifk | 1.15 | 6.26 | 13.68 |
| 18:30 | 3222 | Ghazl EL Mahallah vs Misr Lel Makasa | 1.42 | 4.22 | 7.63 |
| 18:30 | 5528 | Ceramica Cleopatra vs Talaea El Gaish | 2.67 | 2.57 | 3.22 |
| 18:45 | 4802 | Pecs MFC vs Diosgyori Vtk | 2.80 | 3.29 | 2.28 |
| 19:00 | 1175 | Ranheim vs Bryne | 1.53 | 4.12 | 4.91 |
| 19:00 | 2473 | Sandecja vs GKS Tychy | 2.29 | 3.20 | 2.85 |
| 19:00 | 4097 | Aasane Fotball vs Mjondalen | 2.46 | 3.39 | 2.51 |
| 19:00 | 4546 | Sectzya Nes Ziona vs Ironi Kiryat Shmona | 3.34 | 3.44 | 1.96 |
| 19:00 | 4751 | Raufoss vs Kongsvinger IL | 2.11 | 3.43 | 2.99 |
| 19:00 | 5704 | Kfum Oslo vs Fredrikstad | 1.70 | 3.93 | 3.88 |
| 19:15 | 3403 | Sivasspor vs Alanyaspor | 2.51 | 3.32 | 2.67 |
| 19:15 | 4085 | Istanbulspor vs Konyaspor | 3.46 | 3.41 | 2.03 |
| 19:30 | 3278 | Dinamo Brest vs Neman Grodno | 4.91 | 3.58 | 1.62 |
| 19:30 | 4606 | Le Mans vs Sedan | 1.90 | 3.38 | 3.82 |
| 19:30 | 4935 | Qatar SC vs AL Wakrah | 4.51 | 3.73 | 1.64 |
| 19:30 | 5137 | Farul Constanta vs Voluntari | 1.88 | 3.30 | 4.10 |
| 19:30 | 5167 | Roma vs Cremonese | 1.24 | 5.58 | 10.96 |
| 20:00 | 1883 | Kalmar vs IFK Goteborg | 1.97 | 3.24 | 3.54 |
| 20:00 | 2046 | Zwickau vs Bayreuth | 2.09 | 3.45 | 3.20 |
| 20:00 | 2153 | Odense vs Horsens | 2.22 | 3.31 | 3.11 |
| 20:00 | 2569 | Angelholms vs IFK Malmo | 1.25 | 5.51 | 8.46 |
| 20:00 | 3140 | Sirius FK vs BK Hacken | 3.78 | 3.78 | 1.75 |
| 20:00 | 3165 | Penafiel vs Belenenses | 2.00 | 3.33 | 3.53 |
| 20:00 | 5440 | Bohemians vs Hradec Kralove | 2.10 | 3.37 | 3.47 |
| 20:10 | 5936 | Hammarby vs Degerfors | 1.19 | 6.30 | 9.84 |
| 21:00 | 1426 | Mezokovesdi SE vs Debreceni VSC | 2.25 | 3.34 | 2.80 |
| 21:00 | 1954 | Ponferradina vs UD Ibiza Eivissa | 2.09 | 3.21 | 3.46 |
| 21:00 | 2866 | Jong AZ Alkmaar vs Almere City | 3.39 | 3.69 | 1.93 |
| 21:00 | 3410 | Coca Cola vs Pyramids | 4.82 | 3.31 | 1.77 |
| 21:00 | 3985 | Leiknir vs KR Reykjavik | 3.63 | 3.78 | 1.79 |
| 21:00 | 4457 | Jong PSV vs Heracles Almelo | 3.38 | 3.63 | 1.95 |
| 21:00 | 5003 | Jong Ajax vs De Graafschap | 2.37 | 3.59 | 2.59 |
| 21:00 | 5078 | Denizlispor vs Caykur Rizespor | 3.43 | 3.43 | 1.93 |
| 21:00 | 5739 | Elche vs Almeria | 2.41 | 3.13 | 2.98 |
| 21:15 | 2039 | ND Gorica vs Domzale | 3.14 | 3.28 | 2.10 |
| 21:45 | 1406 | Sampdoria vs Juventus | 4.96 | 3.67 | 1.65 |
| 21:45 | 2319 | Grenoble Foot vs Bordeaux | 2.90 | 3.00 | 2.49 |
| 21:45 | 4694 | Fenerbahce vs Adana Demirspor | 1.61 | 4.11 | 4.71 |
| 22:00 | 1861 | Manchester Utd vs Liverpool | 4.60 | 4.20 | 1.60 |
| 22:15 | 2449 | Fram Reykjavik vs Breidablik | 4.42 | 4.13 | 1.58 |
| 22:15 | 4410 | Gil Vicente vs Famalicao | 2.19 | 3.31 | 3.16 |
| 22:30 | 3836 | Rosario Central vs Banfield | 2.44 | 2.94 | 2.85 |
| 23:00 | 3377 | Malaga vs Las Palmas UD | 2.60 | 2.95 | 2.80 |
| 23:00 | 3922 | Girona vs Getafe | 2.67 | 2.78 | 2.98 |
| 23:00 | 4763 | Universitario Popayan vs Leones FC | 3.20 | 3.10 | 2.15 |
| 23:15 | 5375 | Vikingur Reykjavik vs Valur | 1.98 | 3.63 | 3.14 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Jumatatu Agosti 22, 2022

Nipashe



Arteta: Huyu Jesus atawatesa sana tu UKURASA 21

# Dejan: Simba mtafurahia sana mabao

●●● Zoran naye amfungukia, huku kiungo 'mkata umeme' kutoka Nigeria akitua...

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufungua akaunti yake ya mabao Simba kwenye Ligi Kuu Bara, mshambuliaji Dejan Georgijevic, amewaahidi mambo mazuri zaidi mashabiki wa timu hiyo kwa kueleza kwamba atahakikisha anapambana kukata kiu yao kwa kile wanachokitaka msimu huu.

**Dejan ambaye juzi alirejesha imani kwa mashabiki wa Simba ambao walikuwa naye bega kwa bega wakimpa sapoti alipokuwa akipitia changamoto ya kuzoea kikosini hapo, aliifungia timu yake bao la pili wakati ikiibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Kagera Sugar katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.**

Katika mchezo huo, Dejan aliingia kipindi cha pili zikiwa zimesalia dakika 20 mechi kumalizika akichukua nafasi ya Moses Phiri aliyeipatia Simba bao la kwanza na kuamsha shangwe dakika ya 81 baada ya kipa wa Kagera kushindwa kucheza krosi iliyochongwa kutoka winga ya kulia.

Mshambuliaji huyo baada ya kunasa mpira aligeuka kwa haraka na kupiga shuti kali kwa mguu wa kushoto lililotinga nyavuni huku likiwapita mabeki wawili wa Kagera Sugar.

Akizungumza na gazeti hili jana, Dejan alisema amefurahi kufunga bao lake la kwanza ndani ya Simba, na kwamba atahakikisha anafunga zaidi.

Alisema hakuwa na presha yoyote na hakuwa na hofu kwa sababu anatambua uwezo wake na kuahidi kufanya vizuri kila anapopata nafasi ataitumia ipasavyo kwa ajili ya kuwapa furaha mashabiki wao.

"Najua mashabiki wanachokitaka kutoka kwangu, nawashukuru kwa kunitia moyo, sitawaangusha kwani nitaendelea kutimiza kile wanachokitaka uwanjani," alisema Dejan.

Katika hatua nyingine, chanzo chetu cha uhakika ndani ya Simba kimetueleza kwamba klabu hiyo imefanikiwa kupata huduma ya kiungo mkabaji Morice Chukwu kutoka Klabu ya Akwa United ya kwao Nigeria ambaye atatambulishwa muda wowote kuanzia sasa.

"Dili la Mnageria huyo (Chukwu) limekamilika na anatua nchini kesho (leo) kwa ajili ya taratibu zingine na kuingia kambini kujiunga na kikosi kinachoendelea na maandalizi ya michezo ijayo ukiwamo wa Ligi ya Mabingwa Afrika dhidi ya Big Bullets ya Malawi," alisema mtoa habari huyo.

Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, kuhusu suala la usajili alisema bado wanaendelea hawajamaliza kuboresha timu yao kulingana na mahitaji ya kocha wao baada ya kuona mapungufu ya kikosi chake kwa muda ambao amekaa nacho.

"Licha ya kufunga usajili, tulimpa nafasi kocha (Zoran Maki) kuangalia mahitaji yake kama anaona anahitaji kuongezewa mtu basi pesa zipo tutafanya hivyo, akiona mchezaji aliyekuwa kwenye kikosi anatakiwa kuuzwa basi tutafanya hivyo, ili mradi tufanye maboresho ya kikosi chetu.

"Mmeona usajili wetu unaanza kujibu hasa ukiangalia pale mbele kuna Moses Phiri, Augustine Okrah, Mzungu (Dejan) ambaye wote hao mmeona faida yao.

"Kazi ndio imeanza, mzungu wetu hajafunga tu, lakini kafunga bao zuri, Kagera Sugar imekuwa timu ya kwanza kufungwa na mzungu, tunakoelekea kuna maafa makubwa yanakuja, mlete mzungu, anajua huyo, ana hatari huyo, hatujamaliza," Ahmed.

Kwa upande wa Kocha Mkuu, Zoran Maki akimzungumzia Dejan, alisema bado anahitaji muda na kitendo cha kufunga bao la kwanza litamjenga kisaikolojia na kujiamini zaidi katika michezo iliyopo mbele yao.




# Nabi ajivunia fiziki ya wachezaji Yanga

**Na Adam Fungamwango**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi, amesifu utimamu wa mwili wa wachezaji wake, akisema ndicho chanzo kikuu cha kupata ushindi kwenye mechi yake dhidi ya Coastal Union.

Akizungumza juzi baada ya mechi ya raundi ya pili ya Ligi Kuu Tanzania Bara kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha, timu yake ikishinda mabao 2-0 dhidi ya Coastal Union, Nabi alimsifu kocha wa viungo wa timu hiyo kwa kuwafanya wachezaji wake kuwa na stamina pamoja na pumzi ya kutosha, kwani aliona wapinzani wao wakiwa wamechoka dakika 20 za mwisho.

"Kocha wangu wa viungo anafanya kazi kubwa sana, dakika kama 20 hivi za mwisho Coastal Union walichoka, lakini sisi tulibaki na pumzi na fiziki ile ile. Mchezo ulikuwa mzuri, lakini mgumu kwa sababu tulicheza na timu ngumu, na tulilijua hilo, lakini ikumbukwe tumecheza mechi tatu kwa siku saba, miili ya wachezaji imechoka, na uwanja si rafiki sana, kilichotusaidia kwa kiasi kikubwa zaidi ni utimamu wa mwili wa wachezaji wangu," alisema kocha huyo.

Aliwasifu pia wachezaji wake kwa kujitambua na kupambana kwa ajili ya kuzisaka pointi tatu kwa njia ambayo haikuwa rafiki sana. Kwa upande wa Kocha wa Coastal Union, Juma Mgunda, alisema wamepoteza mechi kutokana na uzembe wa mabeki wake.

"Tumefanya makosa, kama unacheza na wachezaji wazoefu na uwezo mkubwa kwa makosa yale ni lazima wakuadhibu. Nina vijana wazuri ambao wanahitaji muda wa kuwatengeneza," alisema Mgunda.

Ni ushindi unaowaweka kwenye nafasi ya pili ya msimamo wa Ligi Kuu, ikiwa na pointi sita mabao manne, ikiruhusu bao moja, huku Coastal Union ikibaki na pointi tatu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >